BENKI KUU YA TANZANIA

# TATHMINI YA MWENENDO WA UCHUMI

Novemba 2025

Yaliyomo

1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia ..... 1

2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa ..... 3

2.1 Mfumuko wa Bei ..... 3

2.2 Sera ya Fedha ..... 6

2.3 Viwango vya Riba ..... 8

2.4 Masoko ya Fedha ..... 8

2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ..... 9

2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa ..... 10

2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje ..... 12

VIAMBATISHO ..... 19

# 1.0 Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Ripoti ya Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF) iliyotolewa mwezi oktoba 2025 inaonyesha marekebisho madogo ya juu ya makadirio ya ukuaji  wa uchumi wa dunia ikilinganishwa na toleo la mwezi Aprili 2025. Uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.2 mwaka 2025, kutoka makadirio ya awali ya asilimia 2.8, ingawa ni kiwango cha chini kuliko ukuaji wa asilimia 3.3 mwaka 2024. Hali hii imechangiwa na kuboreka kwa mazingira ya kibiashara na kifedha, pamoja na ongezeko la uwekezaji katika teknolojia ya Akili Mnemba (Artificial Intelligence), hususan Marekani na Uchina[1]. Aidha, kupungua kwa hali ya kutokutabirika kwa sera za uchumi na biashara duniani kumeimarisha zaidi matarajio ya ukuaji wa uchumi wa dunia (Vielelezo 1.1a na 1.1b).

Mfumuko wa bei ulionyesha mwenendo mchanganyiko, lakini kwa ujumla ulipungua mwezi Oktoba 2025 (Kielelezo 1.2). Viwango vya mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea viliendelea kushuka vikikaribia malengo ya muda wa kati, huku kukiwa na maendeleo ya kurithisha katika Ukanda wa Euro na Uingereza. Mfumuko wa bei nchini Marekani uliendelea kubaki juu ya lengo. Kwa upande wa nchi zinazoibukia kiuchumi, mfumuko wa bei ulipungua, ukichangiwa zaidi na mbinyo wa sera ya fedha, hali bora ya ugavi wa bidhaa na huduma, kuporomoka kwa mfumuko wa bei uliokuwa kwenye viwango vya karibu na sifuri nchini China. Katika Ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC) mfumuko wa bei kwa nchi nyingi uliendelea kubakia ndani ya viwango vya utangamano wa kikanda (Vielelezo1.3 na 1.4). Hali hii imewezesha benki kuu katika nchi nyingi aidha ziliendelea kubakiza au kupunguza viwango vya riba, sambamba na malengo mapana ya uchumi.

**Kielelezo 1.1a: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Sera za Dunia**




Chanzo: https://www.policyuncertainity.com/trade

**Kielelezo 1.1b: Fahirisi ya Kutokuwa na Uhakika wa Biashara Duniani**




Chanzo: https://worlduncertainityindex.com/

[1] https://www.imf.org/en//media/files/publications/weo/2025/october/english/text.pdf

**Kielelezo 1.2: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazochipukia Kiuchumi**




Chanzo: Bloomberg

**Kielelezo 1.3: Mfumuko wa Bei Katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa (inflation target)

**Kielelezo 1.4: Mfumuko wa Bei Miongoni mwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika**



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Tanbihi: Mistari ya nukta inaashiria viwango vya mfumuko wa bei vilivyokusudiwa

**Kielelezo 1.5: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia**




Chanzo: http://www.worldbank.org/prospects
Tanbihi: DAP Inaashiria Di-ammonium phosphate

Bei za bidhaa duniani ziliendelea kuonyesha mwenendo tofauti (Kielelezo 1.5 na Jedwali 8A).

Katika masoko ya nishati, bei za mafuta ghafi zilipungua mwezi Oktoba 2025 ikilinganishwa na mwezi uliotangulia, hali hii ilitokana na uzalishaji wa ziada kwa nchi zinazozalisha mafuta (nchi wanachama wa OPEC+ na zisizo wanachama wa OPEC+) na kupungua kwa uhitaji. Wakati huohuo, mahitaji ya dhahabu yalipanda na kufikia

kiwango cha juu zaidi, yakichochewa na matarajio ya kupunguzwa kwa kiwango cha riba na Benki Kuu ya Marekani.

Mabadiliko ya bei za bidhaa za kilimo yalikuwa yenye mwenendo tofauti (Kielelezo 1.5 na Jedwali 8A). Bei za nishati zilipungua huku bei mafuta ghafi ilishuka kutokana na ziada ya usambazaji na mahitaji hafifu, wakati dhahabu ilipanda hadi kiwango cha kihistoria kutokana na matarajio ya kulegezwa kwa sera za kifedha za Marekani.

Bei za kahawa (Robusta na Arabica) zilipanda kutokana na upungufu wa usambazaji uliosababishwa na hali mbaya ya hewa nchini Brazil na Vietnam. Bei za mafuta ya mawese pia ziliongezeka kutokana na ongezeko la mahitaji kutoka nchi za Asia, licha ya kuongezeka kwa uzalishaji nchini Malaysia na Indonesia. Vilevile, bei za mahindi zilipanda licha ya kuongezeka kwa upatikanaji duniani, zikichochewa na makubaliano ya kibiashara kati ya Marekani na China yaliyoongeza mahitaji. Aidha, bei za ngano zilipungua kutokana na ziada ya usambazaji kufuatia mavuno mazuri nchini Marekani, Urusi na Umoja wa Ulaya [2]. Bei za sukari zilipungua kutokana na matarajio ya ongezeko la usambazaji kufuatia mavuno mazuri ya miwa nchini Brazil na India—nchi zinazozalisha sukari kwa wingi duniani. Bei za mbolea zilishuka kutokana na ongezeko la uzalishaji nchini Morocco na Saudi Arabia, kwa viwango vilivyofidia vizuizi vya mauzo ya mbole kutoka China[3].

# 2.0 Mwenendo wa Uchumi wa Taifa

## 2.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu na ndani ya wigo wa kitaifa wa asilimia 3–5, sambamba na viwango vya utangamano wa SADC na EAC (Kielelezo 2.1.1).

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2025, mfumuko wa bei wa jumla uliongezeka kwa kiasi kidogo na kufikia asilimia 3.5 kutoka asilimia 3.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, hali iliosababishwa na kupanda kwa bei za baadhi ya bidhaa za chakula (Jedwali 2.1.1). Aidha, mwenendo huu tulivu wa mfumuko wa bei ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha, uratibu mzuri kati ya sera za fedha na za bajeti, pamoja na maendeleo endelevu ya mageuzi ya kimuundo yanayolenga kuhakikisha upatikanaji wa chakula cha kutosha.

Maoteo ya mfumuko wa bei yanaonyesha mwenendo wake kuendelea kubaki ndani ya wigo wa malengo ya kitaifa ambao hautofautiani sana na mwenendo wa hivi karibuni. Hatari ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei inabaki kuwa ndogo kutokana na utekelezaji thabiti wa sera za fedha, matarajio ya upatikanaji wa chakula cha kutosha, uthabiti wa kiwango cha ubadilishaji wa fedha, pamoja na utulivu wa bei za nishati katika soko la dunia (Jedwali 2.1.1).

[2] Ripoti ya Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), Makadirio ya Uzalishaji na Mahitaji ya Kilimo Duniani – Novemba 2025 ilionesha kuwa uzalishaji wa ngano ulifikia tani milioni 1,009.91, ongezeko kutoka tani milioni 994.94 mwaka uliotangulia

[3] China hupunguza usafirishaji wa mbolea nje ya nchi katika miezi ya kuelekea msimu wa upandaji wa ndani ili kuipa kipaumbele upatikanaji wa mbolea kwa matumizi ya ndani na kudhibiti bei.

## Jedwali 2.1.1: Maendeleo ya Mfumuko wa Bei

2020 = 100

| Makundi Makuu ya Fahirisi | Mizania | Badiriko la Mfumuko wa bei (Asilimia) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Badiriko: Mwezi hadi Mwezi | | | Badiriko kwa Mwaka | | |
| | | Okt-24 | Sep-25 | Okt-2025 | Okt-2024 | Sep-25 | Okt-2025 |
| Vyakula na Vinywaji Baridi | 28.2 | -0.5 | -0.6 | -0.2 | 2.5 | 7.0 | 7.4 |
| Vinywaji Vikali na Tumbaku | 1.9 | 0.0 | 0.6 | 0.0 | 2.3 | 3.6 | 3.6 |
| Nguo, Mavazi na Viatu | 10.8 | -0.1 | 0.3 | 0.1 | 2.0 | 1.9 | 2.0 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati zinginezo | 15.1 | -0.6 | 0.3 | -0.5 | 5.4 | 2.3 | 2.4 |
| Makazi | 7.9 | 0.0 | 0.6 | 0.3 | 2.1 | 2.8 | 3.1 |
| Afya | 2.5 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 1.8 | 1.2 | 1.2 |
| Usafiri | 14.1 | -0.3 | 0.9 | -0.7 | 3.6 | 2.1 | 1.7 |
| Habari na Mawasiliano | 5.4 | 0.0 | 0.0 | 0.1 | 1.3 | 0.2 | 0.3 |
| Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.6 | -0.1 | -0.1 | 0.0 | 2.3 | 0.8 | 1.0 |
| Elimu | 2.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 3.1 | 2.9 | 3.0 |
| Migahawa na Huduma za Malazi | 6.6 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 2.7 | 1.0 | 1.0 |
| Bima na Huduma za Kifedha | 2.1 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 1.3 | 0.4 | 0.4 |
| Huduma Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidha na Huduma Mchanganyiko | 2.1 | 0.5 | 0.0 | -0.2 | 6.4 | 2.3 | 1.6 |
| Fahirisi Bidhaa Zote | 100.0 | -0.3 | 0.1 | -0.2 | 3.0 | 3.4 | 3.5 |
| Makundi Mengine Teule | | | | | | | |
| Faharisi ya Bidhaa za Msingi | 73.9 | -0.1 | 0.3 | -0.1 | 3.2 | 2.2 | 2.1 |
| Fahirisi Isiyojumuisha Fahirishi za Bidhaa za Msingi | 26.1 | -0.9 | -0.5 | -0.4 | 2.4 | 6.7 | 7.3 |
| Fahirisi za Mafuta, Nishati na Bili za Maji | 5.7 | -1.7 | 0.9 | -1.4 | 9.7 | 3.7 | 4.0 |
| Fahirisi za Huduma | 37.2 | -0.1 | 0.4 | -0.3 | 2.2 | 1.3 | 1.0 |
| Fahirisi za Bidhaa | 62.8 | -0.4 | -0.1 | -0.1 | 3.5 | 4.7 | 5.0 |
| Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu | 4.1 | -0.2 | 0.1 | -0.2 | 2.9 | 2.5 | 2.6 |
| Fahirisi za Bidhaa zote Isipokuwa Chaakula na Vinywaji  Visivyo na Kilevi | 71.8 | -0.2 | 0.4 | -0.2 | 3.2 | 1.9 | 1.9 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

## Kielelezo 2.1.1: Mfumuko wa bei na malengo yake

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mfumuko wa bei za vyakula ulikua kwa asilimia 7.4 mwezi Oktoba 2025, ukipanda kutoka asilimia 2.5 mwezi Oktoba 2024, hali iliyochochewa zaidi na ongezeko la bei za vyakula vya msingi kama vile mahindi, mchele, ulezi na mtama (Kielelezo 2.1.2a na 2.1.2b). Isipokuwa kwa Septemba 2025, mfumuko wa bei wa vyakula visivyosindikwa umeendelea kuwa kichocheo kikuu cha mfumuko wa bei wa jumla tangu Juni 2025 (Kielelezo 2.1.3).

## Kielelezo 2.1.2: Kiwango cha Mfumuko wa Bei za Mazao

### a. Mazao ya vyakula vikuu

asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchambuzi wa Benki Kuu

### b. Mazao vyakula mbadala

Asilimia




Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara, na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 2.1.3: Mchango katika mfumuko wa bei

asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

**Kielelezo 2.1.4: Viwango vya mfumuko wa bei kwa miezi kumi na mbili.**

asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Uchanganuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Kiwango cha mfumuko wa bei wa fahirisi za msingi kilipungua hadi asilimia 2.1 kwa mwezi Oktoba 2025 kutoka asilimia 3.2 kwa mwezi kama huo 2024. Mfumuko wa bei za nishati, mafuta na huduma za msingi ulipanda hadi asilimia 4 mwezi Oktoba 2025, kutoka asilimia 3.7 mwezi uliotangulia, lakini ulikuwa chini ya kiwango cha asilimia 9.7 katika kipindi kwa mwezi Oktoba 2024 (Kielelezo 2.1.4). Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa bei za kuni na mkaa. Aidha, bei za bidhaa za petroli—zikijumuisha petroli, dizeli na mafuta ya taa—ziliendelea kupungua kwa mwezi Oktoba 2025, sambamba na kupungua kwa bei katika soko la dunia (Kielezo 2.1.5).

**Kielelezo 2.1.5: Bei za Bidhaa za Mafuta**

TZS kwa lita




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Tanbihi: Bidhaa nyeupe za petroli huashiria wastani wa bei za Dunia

Hifadhi ya chakula iliyo chini ya Wakala wa Kitaifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) iliendelea kuwa toshelevu, ikiongezeka kwa tani 22,966 hadi kufikia tani 593,485 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia. Hali hii ilisababishwa na ununuzi wa tani 24,399.9 na kuuzwa kwa tani 1,434 za mahindi kwa wafanyabiashara na Shirika la Mpango wa Chakula Ulimwenguni (WFP) (Jedwali 2.1.2).

**Jedwali 2.1.2: Akiba ya Chakula katika Hifadhi ya Chakula.**

Tani

| Kipindi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jan | 43,597 | 110,398 | 207,899 | 124,736 | 270,984 | 646,480 |
| Feb | 41,231 | 110,389 | 203,297 | 106,881 | 326,172 | 619,659 |
| Mac | 39,597 | 109,231 | 200,626 | 80,123 | 336,099 | 587,062 |
| Apr | 38,053 | 109,231 | 190,366 | 63,808 | 340,102 | 557,228 |
| Mei | 38,291 | 108,284 | 149,402 | 51,367 | 340,002 | 509,990 |
| Jun | 52,725 | 107,384 | 141,576 | 46,665 | 340,479 | 477,923 |
| Jul | 90,255 | 107,384 | 140,695 | 94,088 | 368,855 | 485,930 |
| Ago | 92,991 | 123,635 | 144,410 | 210,020 | 489,187 | 537,571 |
| Sep | 109,733 | 150,057 | 149,044 | 244,169 | 651,403 | 570,519 |
| Okt | 110,895 | 192,408 | 151,794 | 244,289 | 708,399 | 593,485 |
| Nov | 110,289 | 209,057 | 147,401 | 244,223 | 702,502 | |
| Des | 110,398 | 214,968 | 137,655 | 248,282 | 677,115 | |

Chanzo: Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula.

## 2.2 Sera ya Fedha

Sera ya fedha imeendelea kuhakikisha mfumuko wa bei unabakia katika kiwango kidogo na tulivu ili kusaidia ukuaji wa uchumi. Katika kikao chake cha Mwezi Oktoba 2025, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) iliendelea kubakiza kiwango cha riba cha msingi (CBR) katika asilimia 5.75. Utekelezaji wa sera ya fedha ulikuwa wa kuridhisha, hali iliochangia kuhakikisha mfumuko wa bei kubaki ndani ya wigo wa kitaifa wa asilimia 3–5. Aidha, hali ya ukwasi katika mabenki iliendelea kuwa ya kuridhisha, ambapo kiwango cha riba cha soko la fedha (IBCM) cha siku 7 kilikuwa wastani wa asilimia 6.28, kiwango kilichokuwa ndani ya wigo wa lengo la ± pointi za asilimia kutoka CBR (Kielelezo 2.2.1). Hali hii ilichangiwa na usimamizi wa ukwasi uliofanywa na Benki kupitia kupitia minada ya *reverse repo* (Kielelezo 2.2.2). Vilevile, Benki iliendesha minada ya hati fungani za muda mfupi (siku 91) ili kuhakikisha kiwango cha ukwasi kinabaki katika hali inayofaa kwa uchumi wakati wote.

**Kielelezo 2.2.1: Riba ya Benki Kuu na wastani wa siku 5 wa Riba ya Mikopo ya Siku 7**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 2.2.2: Mikopo ya muda mfupi kwa mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Kufuatia kuimarika kwa hali ya ukwasi katika uchumi, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M3) ulikua kwa asilimia 21.5 kwa mwezi Oktoba 2025 ikilinganishwa na asilimia 20.4 kwa mwezi uliotangulia na aslimia 14.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Kielelezo 2.2.3 na Jedwali 2.2.1). Ukuaji huu ulichagizwa zaidi na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi ambayo iliendelea kukua kwa asilimia 16.1 kwa mwaka kama ilivyorekodiwa mwezi uliotangulia (Vielelezo 2.2.4 na 2.2.5).

### Kielelezo 2.2.3: Mwenendo wa Ujazi wa Fedha




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Jedwali 2.2.1: Ujazi wa Fedha na Vipengele Vyake

| Kipengele | Kiasi (Shilingi Billioni) Okt-24 | Sep-25 | Okt-25 | Ukuaji kwa mwaka (%) Okt-24 | Sep-25 | Okt-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Rasilimali halisi za nje | 13,773.6 | 15,896.7 | 15,715.4 | 42.3 | 16.0 | 14.1 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 12,668.2 | 14,467.3 | 13,334.3 | 26.9 | 13.0 | 5.3 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | 1,105.4 | 1,429.3 | 2,381.1 | --- | --- | --- |
| Rasilimali halisi za ndani | 35,469.4 | 41,957.4 | 44,091.2 | 6.6 | 22.1 | 24.3 |
| Madai rasmi ya ndani | 48,136.2 | 54,854.2 | 56,509.3 | 9.7 | 16.3 | 17.4 |
| Amana za Serikali zilizopo Ben | 7,837.1 | 8,723.1 | 8,965.9 | -12.7 | 6.8 | 14.4 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 36,517.8 | 41,999.9 | 42,386.9 | 17.0 | 16.1 | 16.1 |
| Rasilimali nyinginezo | -12,666.9 | -12,896.9 | -12,418.1 | 19.4 | 0.8 | -2.0 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 49,243.0 | 57,854.0 | 59,806.6 | 14.6 | 20.4 | 21.5 |
| Amana za fedha za kigeni | 12,745.0 | 13,337.2 | 13,882.1 | 34.2 | 7.3 | 8.9 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2) | 36,498.0 | 44,516.8 | 45,924.5 | 9.1 | 24.9 | 25.8 |
| Amana zinginezo | 14,224.2 | 16,600.4 | 16,848.4 | 10.3 | 20.2 | 18.4 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 22,273.8 | 27,916.4 | 29,076.1 | 8.3 | 27.9 | 30.5 |
| Ujazi wa fedha ulio kwenye mzungukc | 7,408.2 | 7,730.8 | 8,428.1 | 17.3 | 5.1 | 13.8 |
| Amana za hundi | 14,865.6 | 20,185.6 | 20,648.0 | 4.3 | 39.5 | 38.9 |
| Fedha za msingi (M0) | 11,765.8 | 13,717.6 | 15,086.7 | 19.8 | 23.2 | 28.2 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.4: Mabadiliko katika vyanzo vya ujazi wa fedha kwa mwaka




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 2.2.5: Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

Katika mwezi Oktoba 2025, shughuli za uchimbaji madini ziliendelea kuwa na kasi kubwa ya ukuaji wa mikopo wa asilimia 29.7, zikifuatiwa na shughuli za kilimo (asilimia 25.6) na hoteli na migahawa 23.2 (Jedwali 2.2.2). Mikopo kwa shughuli binafsi ambayo hutumika kugharamia shughuli ndogo sana, ndogo na za kati iliendelea kuwa sehemu kubwa ya mikopo ya sekta binafsi, kwa asilimia 36.4, biashara (asilimia 13.2) na kilimo (asilimia 12.9) (Kielelezo 2.2.6).

### Jedwali 2.2.2: Ukuaji wa Mikopo kwa Shughuli za kiuchumi

Asilimia

| | Oct-24 | Nov-24 | Des-24 | Mac-25 | Apr-25 | Mei-25 | Jun-25 | Jul-25 | Ago-25 | Sep-25 | Ókt-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uchimbaji Madini | 5.7 | 4.0 | -36.3 | -24.8 | -10.5 | 22.9 | 20.8 | 0.8 | 3.2 | 32.4 | 29.7 |
| Kilimo | 44.7 | 41.9 | 41.0 | 36.3 | 29.8 | 29.8 | 30.2 | 31.8 | 30.1 | 27.6 | 25.6 |
| Hoteli na migahawa | -3.0 | -1.5 | 2.7 | 5.4 | 7.0 | 21.7 | 22.5 | 13.0 | 11.4 | 16.3 | 23.2 |
| Biashara | 6.6 | 6.7 | 5.6 | 12.7 | 14.4 | 24.1 | 21.3 | 26.2 | 29.2 | 24.8 | 21.8 |
| Uchukuzi na mawasiliano | 18.6 | 11.3 | 13.2 | 22.4 | 23.8 | 25.6 | 25.7 | 18.9 | 18.8 | 17.4 | 18.7 |
| Ujenzi | 17.8 | 16.6 | 11.6 | 35.1 | 39.2 | 27.9 | 25.7 | 21.6 | 14.8 | 15.7 | 14.2 |
| Shughuli binafsi | 18.7 | 19.2 | 14.7 | 9.4 | 14.7 | 13.6 | 13.7 | 13.1 | 15.0 | 14.7 | 11.3 |
| Viwanda | 13.4 | 9.4 | 16.3 | 10.9 | 7.7 | 7.3 | 2.5 | 6.3 | 3.4 | 0.1 | 5.2 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

**Kielelezo 2.2.6: Mchango wa Shughuli za kiuchumi katika Ukuaji wa Mikopo**

Asilimia




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.3 Viwango vya Riba

Riba za mikopo na amana ziliendelea kuwa tulivu, zikiwa na mabadiliko madogo katika mwezi Oktoba 2025. Riba za mikopo zilifikia wastani wa asilimia 15.19 mwezi Oktoba, 2025 takriban sawa na asilimia 15.18 iliyorekodiwa mwezi Septemba 2025 (Jedwali 2.3.1). Riba za mikopo inayotolewa kwa wateja wakubwa zilipungua hadi asilimia 12.40 ikilinganishwa na asilimia 12.84 kwa mwezi uliotangulia.

Wakati huohuo, riba za amana zilipungua hadi wastani wa asilimia 8.36 kutoka asilimia 8.50 Septemba 2025, huku riba za amana kwa wateja wakubwa zilibakia takriban asilimia 11.22 kama ilivyokuwa mwezi uliotangulia. Kufuatia mwenendo huu, wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja uliongezeka hadi asilimia 6.28, kutoka asilimia 5.65 mwezi kama huo mwaka 2024.

**Jedwali 2.3.1: Riba za Amana na Mikopo Inayotolewa Benki za Biashara**

Asilimia

| | Okt-24 | Des-24 | Mac-25 | Apr-25 | Mei-25 | Jun-25 | Jul-25 | Ago-25 | Sep-25 | Okt-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba za amana | 2.85 | 2.84 | 2.86 | 2.89 | 2.52 | 2.90 | 2.90 | 2.90 | 2.92 | 2.93 |
| Riba ya mikopo - jumla | 15.67 | 15.71 | 15.50 | 15.16 | 15.18 | 15.23 | 15.16 | 15.07 | 15.18 | 15.19 |
| Riba za mikopo (mwaka 1) | 16.06 | 15.74 | 15.83 | 16.15 | 15.96 | 15.69 | 15.51 | 15.64 | 15.52 | 15.50 |
| Riba za mikopo (wateja wakubwa) | 12.93 | 12.83 | 12.94 | 12.88 | 12.99 | 12.68 | 12.56 | 12.72 | 12.84 | 12.40 |
| Riba za amana -jumla | 8.25 | 8.33 | 8.00 | 7.82 | 8.58 | 8.74 | 8.83 | 8.61 | 8.50 | 8.36 |
| Riba za amana (miezi 12) | 10.41 | 9.62 | 8.14 | 9.27 | 9.72 | 9.79 | 9.88 | 9.99 | 9.84 | 9.21 |
| Riba za amana (wateja wakubwa) | 10.27 | 10.39 | 10.35 | 10.52 | 10.64 | 11.21 | 10.72 | 10.99 | 11.05 | 11.22 |
| Tofauti kati ya riba za mikopo na amana | 5.65 | 6.12 | 7.69 | 6.88 | 6.24 | 5.90 | 5.63 | 5.66 | 5.69 | 6.28 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na mabenki

## 2.4 Masoko ya Fedha

## Soko la dhamana za Serikali

Katika mwezi Oktoba 2025, Benki Kuu iliendesha minada miwili ya dhamana za Serikali za muda mfupi yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 162.7. Kiasi kikubwa cha dhamana hizi kilikuwa kwa ajili ya kugharamia matumizi Serikali, huku kiwango kidogo kikiwa kwa ajili ya utekelezaji wa sera ya fedha. Sanjari na uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi, minada ilipokea zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 299.2, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi billion 128.0 zilikubaliwa. Kufuatia mwenendo huu, riba za dhamana za Serikali ziliongezeka kidogo hadi wastani wa asilimia 6.27 kutoka asilimia 6.03 mwezi uliotangulia (Kielelelzo 2.4.1).

**Kielelezo 2.4.1: Mwenendo wa minada ya dhamana za Serikali**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Vilevile, Benki iliendesha minada ya hati fungani za miaka 2 na 10, yenye thamani ya shilingi bilioni 119.2, na 144.6, mtawalia. Hati hizi zilikuwa na mahitaji makubwa kuliko

ilivyotarajiwa sanjari na uwepo wa ukwasi wa kutosha na wawekezaji kupendelea zaidi hati fungani kutokana na kuongezeka kwa uelewa.Jumla ya zabuni zilizowasilishwa kwa minada yote miwili ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 670.5, ambapo zabuni zenye thamani ya shilingi bilioni 231.4 zilikubaliwa. Riba za hati fungani za miaka 2 na 10 zilipungua hadi asilimia 10.55 na 12.55, mtawalia.

## Soko la fedha baina ya mabenki

Soko la fedha baina ya mabenki liliendelea kurahisisha usambazaji wa ukwasi wa shilingi kati ya mabenki. Jumla ya mauzo kwa mwezi Oktoba 2025 ilipungua hadi shilingi bilioni 2,255.4 kutoka shilingi bilioni 3,261.6 mwezi uliotangulia huku mikopo ya siku saba ikiendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote, ikiwa ni zaidi ya asilimia 75.4 (Kielelezo 2.4.2). Sanjari na uwepo wa ukwasi wa kutosha, wastani wa riba ya mikopo katika soko ulipungua hadi asilimia 6.38 kutoka asilimia 6.45 mwezi Septemba 2025.

**Kielelezo 2.4.2: Mwenendo wa Soko la Fedha Baina ya Mabenki**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Soko la Fedha za Kigeni

Hali ya soko la fedha za kigeni iliendelea kuwa tulivu, kukiwa na kiwango cha kutosha cha fedha za kigeni, kilichochangiwa na mapato yatokanayo na mauzo ya dhahabu na mazao ya biashara nje ya nchi, pamoja na huduma za utalii. Kufuatia mwenendo huu, mauzo ya fedha za kigeni katika soko yalifikia dola za Marekani milioni 133.7, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 93.8 mwezi Septemba 2025, ambapo asimilia 66.9 ya mauzo haya yalifanywa na benki za biashara. Wakati huohuo, Benki Kuu ilishiriki katika soko kwa mujibu wa sera ya ushiriki katika soko la fedha za kigeni ili kupunguza mabadiliko makubwa yasiyo ya kawaida, kwa kuuza dola za Marekani milioni 44.2 (Kielelezo 2.4.3).

Shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa imara, ikibadilishwa kwa wastani wa Shilingi 2,460.54 kwa dola moja ya Marekani, kutoka Shilingi 2,471.69 kwa dola moja ya Marekani kwa mwezi uliotangulia na kubakia imara dhidi ya sarafu kubwa nyingine. Hii ilikuwa sawa na ongezeko la thamani kwa asilimia 9.5 kwa mwaka ikilinganishwa na kushuka kwa thamani ya shilingi kwa asilimia 8.9 mwezi Oktoba 2024.

**Kielelezo 2.4.3: Mwenendo wa Soko la Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika mwezi wa Septemba 2025 uliendelea kuwa imara, ukizidi makadirio ya mwezi huo kwa asilimia 6.1 kufikia shilingi bilioni 3,718.2. Kati ya kiasi hiki, Serikali Kuu ilikusanya shilingi bilioni 3,570.4, ikivuka lengo la mwezi Septemba 2025 kwa

asilimia 6.5. Bakaa la shilingi bilioni 147.8 lilikuwa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mapato ya kodi yaliendelea kufanya vizuri, yakivuka lengo lililowekwa kwa asilimia 11.4 kufikia shilingi bilioni 3,124.1. Mafanikio haya ni matokeo ya maboresho yanayoendelea katika utendaji kazi wa Mamlaka ya Mapato (TRA). Kwa upande mwingine, mapato yasiyo ya kodi yalikuwa chini ya lengo la shilingi bilioni 548 kwa shilingi bilioni 101.9 bilioni (Kielelezo 2.5.1).

**Kielelezo 2.5.1: Mapato ya Serikali Kuu Mwezi Septemba 2025**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2025 ni za awali

Serikali imeendelea kutekeleza bajeti yake kulingana na upatikanaji wa mapato. Jumla ya matumizi ya Serikali kwa mwezi Septemba 2025 yalikuwa shilingi bilioni 4,284.2. Kati ya kiasi hiki, shilingi bilioni 2,508.6 yalikuwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1,775.6 yalikuwa kwa miradi ya maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa matumizi ya maendeleo, asilimia 82.3 ilitokana na vyanzo vya ndani (Kielelezo 2.5.2).

**Kielelezo 2.5.2: Matumizi ya Serikali Kuu Mwezi Septemba 2025**

Shilingi bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: Takwimu halisi za mwaka 2025 ni za awali

## 2.6 Mwenendo wa Deni la Taifa

Deni la Taifa lilifikia dola za Marekani milioni 50,932.1 mwishoni mwa mwezi Oktoba 2025, likipungua kwa asilimia 0.1 ikilinganishwa na kiwango kilichorekodiwa mwezi u;liotangulia. Kati ya kiasi hicho, asilimia 69.5 lilikuwa deni la nje.

### Deni la Nje

Deni la nje (linalojumuisha deni la Serikali na la sekta binafsi) lilipungua kwa asilimia 0.7 mwishoni mwa mwezi Oktoba 2025 kutoka mwezi uliotangulia, na kufikia dola za Marekani milioni 35,385.5. Kati ya kiasi hicho, asilimia 81.7 lilikuwa deni la nje la Serikali (Jedwali 2.6.1). Mikopo kutoka vyanzo vya nje ya nchi kwa mwezi Oktoba 2025 ilikuwa dola za Marekani milioni 89.9, ambapo sehemu kubwa ilipokelewa na Serikali Kuu. Aidha, kiasi cha dola za Marekani milioni 220.5 kilitumika kulipia deni la nje, ambapo dola za Marekani milioni 169.3 zilitumika kufanya malipo ya deni la msingi na kiasi cha dola za Marekani milioni 51.2 kilitumika kulipia riba.

**Jedwali 2.6.1: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopaji**

Dola za Marekani Milioni

| Mkopaji | Okt-24 Kiasi | Okt-24 Mchango (%) | Sep-25[r] Kiasi | Sep-25[r] Mchango (%) | Okt-25[p] Kiasi | Okt-25[p] Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | 25,532.7 | 80.5 | 29,157.3 | 81.8 | 28,911.6 | 81.7 |
| Deni ambalo halijalipwa | 25,455.7 | 80.3 | 29,078.6 | 81.6 | 28,832.9 | 81.5 |
| Malimbikizo ya riba | 76.9 | 0.2 | 78.7 | 0.2 | 78.7 | 0.2 |
| Sekta binafsi | 6,167.6 | 19.5 | 6,481.1 | 18.2 | 6,470.2 | 18.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 5,692.4 | 18.0 | 5,871.2 | 16.5 | 5,845.5 | 16.5 |
| Malimbikizo ya riba | 475.2 | 1.5 | 609.9 | 1.7 | 624.7 | 1.8 |
| Mashirika ya umma | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 |
| Deni ambalo halijalipwa | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 | 3.8 | 0.0 |
| Malimbikizo ya riba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Jumla ya deni la nje | 31,704.0 | 100.0 | 35,642.2 | 100.0 | 35,385.5 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali; na TANESCO, ATCL, TRC, TPA, TFC na DAWASA hazina deni la nje ambalo halijalipwa

Muundo wa deni la nje kwa aina ya wakopeshaji kwa mwezi Oktoba 2025 uliendelea kubaki bila mabadiliko makubwa ikilinganishwa na mwezi uliotangulia na kipindi kinacholingana mwaka 2024. Taasisi za kimataifa ziliendelea kushikilia sehemu kubwa ya wakopeshaji kwa asilimia 57.4, zikifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara (Jedwali 2.6.2). Aidha, mikopo iliyopokelewa kama msaada kwa ajili ya urari wa malipo yote ya nje na kugharamia bajeti iliongoza, ikifuatiwa na mikopo kwenda kwenye shughuli za usafirishaji na mawasiliano. Dola ya Marekani iliendelea kuwa sarafu kuu ya deni la nje kwa asilimia 66.2, ikifuatiwa na sarafu ya Umoja wa Ulaya (Jedwali 2.6.3 na 2.6.4).

**Jedwali 2.6.2: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Kundi la Wakopeshaji**

Dola za Marekani Milioni

| Mkopeshaji | Okt-24 Kiasi | Okt-24 Mchango (%) | Sep-25[r] Kiasi | Sep-25[r] Mchango (%) | Okt-25[p] Kiasi | Okt-25[p] Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mashirika ya fedha ya kimataifa | 18,071.3 | 57.0 | 20,335.8 | 57.1 | 20,315.8 | 57.4 |
| Deni ambalo halijalipwa | 18,040.5 | 56.9 | 20,291.1 | 56.9 | 20,268.9 | 57.3 |
| Malimbikizo ya riba | 30.8 | 0.1 | 44.8 | 0.1 | 46.9 | 0.1 |
| Nchi washirika wa maendeleo | 1,224.4 | 3.9 | 1,542.5 | 4.3 | 1,516.2 | 4.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,147.4 | 3.6 | 1,463.8 | 4.1 | 1,437.5 | 4.1 |
| Malimbikizo ya riba | 76.9 | 0.2 | 78.7 | 0.2 | 78.7 | 0.2 |
| Benki za kimataifa za biashara | 11,237.7 | 35.4 | 12,657.0 | 35.5 | 12,444.3 | 35.2 |
| Deni ambalo halijalipwa | 10,950.8 | 34.5 | 12,293.0 | 34.5 | 12,069.6 | 34.1 |
| Malimbikizo ya riba | 286.8 | 0.9 | 364.0 | 1.0 | 374.7 | 1.1 |
| Mikopo ya mauzo ya nje | 1,170.7 | 3.7 | 1,106.8 | 3.1 | 1,109.3 | 3.1 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,013.2 | 3.2 | 905.7 | 2.5 | 906.2 | 2.6 |
| Malimbikizo ya riba | 157.5 | 0.5 | 201.1 | 0.6 | 203.1 | 0.6 |
| Jumla ya deni la nje | 31,704.0 | 100.0 | 35,642.2 | 100.0 | 35,385.5 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; na p, takwimu za awali

**Jedwali 2.6.3: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa aina ya Matumizi, kwa**

Asilimia

| Shughuli ya uchumi | Okt-24 | Sep-25[r] | Okt-25[p] |
|---|---|---|---|
| Urari wa malipo yote ya nje, na bajeti (BOP and budget support) | 19.1 | 22.6 | 22.7 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 21.7 | 21.9 | 22.0 |
| Kilimo | 4.9 | 5.2 | 5.2 |
| Nishati na madini | 13.5 | 12.8 | 12.8 |
| Viwanda | 3.5 | 2.4 | 2.4 |
| Huduma za jamii na elimu | 20.3 | 19.6 | 19.8 |
| Fedha na bima | 4.6 | 4.2 | 4.2 |
| Utalii | 1.6 | 1.7 | 1.7 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 5.0 | 4.4 | 4.3 |
| Mengineyo | 5.6 | 5.2 | 5.0 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizorekebishwa; p, takwimu za awali

**Jedwali 2.6.4: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Aina ya Sarafu, kwa**

Asilimia

| Sarafu | Okt-24 | Sep-25[r] | Okt-25[p] |
|---|---|---|---|
| Dola ya Marekani | 66.9 | 66.2 | 66.2 |
| Sarafu ya umoja wa Ulaya (Euro) | 16.6 | 17.6 | 17.6 |
| Yuan ya China | 6.2 | 6.3 | 6.4 |
| Sarafu nyinginezo | 10.2 | 9.8 | 9.8 |
| Jumla | 100.0 | 100.0 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha, na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: r inamaanisha takwimu zilizobadilishwa; na p, takwimu za awali

## Deni la Ndani

Deni la ndani la Serikali liliongezeka kwa asilimia 1.8 kwa mwezi Octoba 2025 na kufikia shilingi

bilioni 38,114.8 (Kielelezo 2.6.1). Sehemu kubwa ya deni la ndani la Serikali linaundwa na hati fungani , wakati benki za biashara, mifuko ya hifadhi za jamii, na Benki Kuu ya Tanzania zikikopesha karibu robo tatu ya deni la ndani (Jedwali 2.6.5 na 2.6.6).

**Kielelezo 2.6.1: Deni la Ndani la Serikali Kuu**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Wizara ya Fedha

**Jedwali 2.6.5: Deni la Ndani la Serikali Kuu Kwa Vyanzo vya Mikopo**

Shilingi Bilioni

| | Okt-24 | | Sep-25 | | Okt-25[P] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Dhamana za serikali | 27,900.1 | 84.5 | 32,498.5 | 86.8 | 32,621.7 | 85.6 |
| Dhamana za serikali za muda mfupi | 1,944.3 | 5.9 | 2,058.7 | 5.5 | 2,079.5 | 5.5 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.6 | 135.8 | 0.4 | 135.7 | 0.4 |
| Dhamana za serikali za muda mrefu | 25,768.7 | 78.0 | 30,304.0 | 80.9 | 30,406.4 | 79.8 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 5,123.0 | 15.5 | 4,960.5 | 13.2 | 5,493.1 | 14.4 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 18.4 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Bakaa hasi | 5,104.7 | 15.5 | 4,942.1 | 13.2 | 5,493.1 | 14.4 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 33,023.2 | 100.0 | 37,459.0 | 100.0 | 38,114.8 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali; na madeni mengine yanajumuisha mkopo wa biashara na marejesho ya kodi ya ushuru

**Jedwali 2.6.6: Deni la Ndani la Serikali Kuu Kwa Kundi la Wakopeshaji**

Shilingi Bilioni

| | Okt-24 | | Sep-25 | | Okt-25[P] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) | Kiasi | Mchango (%) |
| Benki za biashara | 9,510.2 | 28.8 | 10,752.0 | 28.7 | 10,899.8 | 28.6 |
| Benki Kuu ya Tanzania | 7,064.7 | 21.4 | 6,750.9 | 18.0 | 7,301.8 | 19.2 |
| Mifuko ya hifadhi ya jamii | 9,003.3 | 27.3 | 10,282.0 | 27.4 | 10,248.3 | 26.9 |
| Kampuni za bima | 1,913.8 | 5.8 | 1,825.1 | 4.9 | 1,839.9 | 4.8 |
| Mifuko maalumu ya Benki Kuu | 420.3 | 1.3 | 780.5 | 2.1 | 749.5 | 2.0 |
| Wengine | 5,110.8 | 15.5 | 7,068.6 | 18.9 | 7,075.4 | 18.6 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 33,023.2 | 100.0 | 37,459.0 | 100.0 | 38,114.8 | 100.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p, takwimu za awali; na “wengine” inajumuisha taasisi za umma, kampuni, watu binafsi, na  na wawekezaji wasio wakazi

Katika mwezi Oktoba 2025, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 327.7 kutoka soko la ndani kupitia uuzaji wa dhamana zake kwa lengo la kuziba nakisi ya bajeti. Katika kiasi hiki, shilingi bilioni 179 zilitokana na mauzo hati fungani na shilingi bilioni 148.7 dhamana za serikali za muda mfupi. (Kielelezo 2.6.2). Malipo ya deni la ndani yalikuwa shilingi bilioni 482.4, yakijumuisha shilingi bilioni 204.6 kama malipo ya deni la msingi na shilingi bilioni 277.9 malipo ya riba.

**Kielelezo 2.6.2: Dhamana za Serikali Zilizotolewa kwa Madhumuni ya Ufadhili wa Bajeti**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## 2.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Hali ya Sekta ya nje ya uchumi imeendelea kuwa ya kuridhisha. Nakisi ya akaunti ya biashara ilipungua hadi dola za Marekani milioni 2,217.8 kwa mwaka uliomalizika Oktoba 2025, ikiwa ni maendeleo makubwa ukilinganisha na dola za Marekeni milioni  2,893.3 zilizorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Jedwali 2.7.1). Hii ilikuwa sawa na asilimia 2.4 ya Pato laTaifa (GDP), kutoka kilele cha zaidi ya asilimia 6 ya GDP mwaka 2022.Uboreshaji huu umechangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la mauzo ya nje. Ongezeko la mauzo ya nje yaliambatana na kupungua kwa uagizaji wa

bidhaa kutokana na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na ongezeko la uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za matumizi ya nyumbani, ambazo awali zilikuwa zinaagizwa kutoka nje. Akiba za fedha za kigeni zinaendelea kuongezeka, zikifikia takriban dola million 6,171.1 mwishoni mwa mwezi Oktoba 2025, zinazotosheleza matumizi ya miezi 4.7 ya uagizaji unaotarajiwa wa bidhaa na huduma, na kuvuka vigezo vya kitaifa na vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) (Kielelezo 2.7.1).

**Jedwali 2.7.1 Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali**

Dola za Marekani Milioni

| | | | | Mwaka ulioishia Oktoba | | | Mabadiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Okt-24 | Sep-25 | Okt-25 | 2023 | 2024 | 2025p | ya asilimia |
| Urari wa bidhaa | -329.3 | -483.1 | -277.2 | -6,011.5 | -5,652.6 | -4,470.1 | -20.9 |
| Zilozouzwa nje* | 928.3 | 1,020.4 | 949.2 | 7,689.5 | 8,461.5 | 10,137.9 | 19.8 |
| Zilizonunuliwa nje | 1,257.6 | 1,503.4 | 1,226.3 | 13,701.0 | 14,114.1 | 14,608.0 | 3.5 |
| Urari wa huduma | 324.37 | 314.3 | 288.2 | 3,352.9 | 4,011.8 | 3,838.8 | -4.3 |
| Mapato | 606.2 | 576.0 | 543.2 | 5,993.9 | 6,672.0 | 6,910.8 | 3.6 |
| Malipo | 281.9 | 261.7 | 254.9 | 2,640.9 | 2,660.1 | 3,072.0 | 15.5 |
| Urari wa bidhaa na huduma | -4.9 | -168.7 | 11.1 | -2,658.6 | -1,640.8 | -631.2 | -61.5 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 1,534.5 | 1,596.4 | 1,492.3 | 13,683.4 | 15,133.5 | 17,048.7 | 12.7 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 1,539.5 | 1,765.1 | 1,481.2 | 16,341.9 | 16,774.3 | 17,679.9 | 5.4 |
| Urari wa malipo wa vitega uchumi | -221.7 | -191.6 | -221.7 | -1,524.1 | -1,803.3 | -2,036.6 | 12.9 |
| Yaliyoingia | 20.3 | 59.9 | 30.9 | 268.0 | 307.2 | 408.8 | 33.1 |
| Yaliyotoka | 242.0 | 251.4 | 252.6 | -1,792.1 | -2,110.5 | -2,445.4 | 15.9 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 31.1 | 19.0 | 15.5 | 674.1 | 550.8 | 450.0 | -18.3 |
| Iliyoingia | 86.8 | 72.0 | 72.1 | 1,149.3 | 1,214.6 | 962.6 | -20.8 |
| ambapo Serikali | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 108.4 | 108.9 | 94.4 | -13.3 |
| Iliyotoka | 55.7 | 52.9 | 56.6 | 475.2 | 663.9 | 512.5 | -22.8 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali | -195.5 | -341.3 | -195.1 | -3,508.6 | -2,893.3 | -2,217.8 | -23.3 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: a- inamaanisha takwimu za awali
*Zinajumuisha marekebisho ya mauzo nje ya nchi ambayo hayajarekodiwa kikamilifu

**Kielelezo 2.7.1 Akiba ya Fedha za Kigeni**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania
Tanbihi: LHS Inaashiria skeli ya mhimili wa kushoto; RHS, Inaashiria skeli ya mhimili wa kulia

## Mauzo ya Nje ya Nchi

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 17,048.7 katika mwaka unaoishia Oktoba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 15,133.5 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo yatokanayo na huduma

Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yalifikia dola za Marekani milioni 10,137.9, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 8,461.5 kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hili lilichangiwa na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, tumbaku, korosho na kahawa (Kielelezo 2.7.2). Mauzo ya dhahabu pekee yaliongezeka kwa asilimia 38.9 hadi dola za Marekani milioni 4,596.5, kutoka dola za Marekani milioni 3,308.9, ikichangiwa zaidi na kuongezeka kwa bei ya dhahabu kwenye soko la dunia. Mauzo ya bidhaa asilia yalifika dola za Marekani milioni 1,438.2, sawa na ongezeko la asilimia 25.2. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya tumbaku na korosho sambamba na mabadiliko ya bei na kiasi kilichouzwa. Mauzo ya nafaka, hususan mahindi na mchele, yaliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 312.5 kutoka dola za Marekani milioni 221.6, kutokana na ongezeko la mahitaji nchi jirani. Kwa mwezi wa Oktoba 2025, mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 949.2 mwaka 2025, kutoka dola za Marekani milioni 928.3 Oktoba 2024, hali iliyochangiwa na ongezeko la mauzo ya dhahabu na bidhaa za viwandani.

**Kielelezo 2.7.2: Mauzo ya Nje ya Bidhaa na Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p- inamaanisha takwimu za awali

Mauzo ya huduma yaliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 6,910.8 kwa mwaka ulioishia Oktoba 2025, kutoka dola za Marekani milioni 6,672 mwaka uliotangulia. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mapato kwenye huduma za usafiri na utalii. Ongezeko la mapato kwenye huduma za kitalii linaashiria ukuaji thabiti wa sekta hiii, huku idadi ya watalii ikiongezeka kwa asilimia 11.4 hadi kufikia watalii 2,324,387. Aidha, mapato ya usafirishaji, hususan mizigo, yalifikia dola za Marekani milioni 2,470.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,260.5 mwaka uliosha Oktoba 2024 (Kielelezo 2.7.3). Kwa mwezi Oktoba 2025, mapato ya huduma yalikuwa dola za Marekani milioni 543.2, yakiwa chini ya dola za Marekani milioni 606.2 katika mwezi Oktoba 2024.

**Kielelezo 2.7.3: Mapato ya Huduma kwa Sekta**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo*:* Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali

## Uagizaji wa Bidhaa na Huduma kutoka nje ya nchi

Kwa mwaka ulioishia Oktoba 2025, uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 17,679.9, kutoka dola za Marekani milioni 16,774.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na uagizaji wa malighafi za viwandani, vyombo vya usafiri, bidhaa za viwandani pamoja na mashine na mitambo (Jedwali 3.3.3). Uagizaji wa mafuta ulipungua kwa asilimia 12.5 na kufikia dola za Marekani milioni 2,394.4, uliochangiwa zaidi na kushuka kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia. Kwa upande wa mwezi wa Oktoba, uagizaji wa bidhaa ulifikia dola za Marekani milioni 1,226.3 mwezi Oktoba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,257.6 mwezi Oktoba 2024.

**Kielelezo 2.7.4: Uagizaji wa Bidhaa na Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi p inamaanisha takwimu za awali.

Malipo ya huduma yalifikia dola za Marekani milioni 3,072 katika mwaka unaoishia Oktoba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,660.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na malipo ya usafirishaji wa mizigo, sanjari na ongezeko la uagizaji bidhaa nje ya nchi (Kielelezo 2.7.5). Kwa mwezi wa Oktoba 2025, malipo ya huduma yalikuwa dola za Marekani milioni 254.9, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 281.9 mwezi Oktoba 2024.

**Kielelezo 2.7.5: Malipo ya Huduma**

Dola za Marekani Milioni




Chanzo: Benki na Benki Kuu ya Tanzania

Tanbihi: Tanbihi: p inamaanisha takwimu za awali

Nakisi ya urari wa vitega uchumi ilifikia dola za Marekani milioni 2,036.6 kwa mwaka ulioishia Oktoba 2025, ikiongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1,803.3 kutoka kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hili lilitokana na malipo yanayotokana na uwekezaji wa moja kwa moja na riba nje ya nchi. Kwa mwezi Oktoba 2025, nakisi ya urari wa vitega uchumi ilifikia dola za Marekani milioni 221.7, kiasi ambacho ni karibu sawa na nakisi iliyorekodiwa mwezi Oktoba 2024.

Urari wa uhamisho wa mali ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 450, ikipungua kutoka milioni 550.8 mwaka uliotangulia, kulikochangi wa zaidi na uhamishaji wa fedha binafsi. Kwa mwezi wa Oktoba 2025, ziada ya urari wa uhamisho wa mali ilikuwa dola za Marekani milioni 15.5, ikipungua kutoka dola za Marekani milioni 31.1 mwezi Oktoba 2024.

# 3. Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar

## 3.1 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei wa jumla ulipungua hadi kufikia asilimia 3.4 kwa mwezi Oktoba 2025 kutoka asilimia 3.5 iliyorekodiwa mwezi uliotangulia, na asilimia 5.8 katika mwezi unaolingana na huo mwaka 2024 (Jedwali 3.1.1 na Kielelezo 3.1.1). Matokeo haya yamesababishwa na kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula na zisizo za chakula.

Mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula kwa mwaka ulipungua hadi kufikia asilimia 6.4 kutoka asilimia 8.2 iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024 hali iliyotokana na upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani pamoja na mazingira mazuri ya viwango vya ubadilishanaji wa fedha za kigeni uliosaidia uagizaji chakula nje ya nchi. Vilevile, mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula ulishuka hadi asilimia 1 kutoka asilimia 4.1 iliyorekodiwa mwezi wa Oktoba 2024 kutokana na kupungua kwa bei za bidhaa za petroli ikiwemo mafuta ya petrol, dizeli, ya taa na gesi ya mitungi. Mfumuko wa bei wa mwezi Oktoba, 2025 ulibaki asilimia 0.1, sawa na kiasi kilichorekodiwa mwezi Oktoba 2024.

**Jedwali 3.1.1: Mwenendo wa mfumuko wa bei**

Kizio: Julai 2022 =100

| Kundi | | Mabadiriko ya Mwezi | | | Mabadiriko ya mwaka | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uzito | Okt-24 | Sep-25 | Okt-25 | Okt-24 | Sep-25 | Okt-25 |
| Vyakula na Vinywaji Visivyo na Kileo | 41.9 | -1.5 | 0.7 | 0.7 | 8.0 | 4.7 | 7.1 |
| Vinywaji vyenye Vileo, Tumbaku na Madawa ya binadamu | 0.2 | 0.4 | 0.0 | -0.2 | 25.1 | 2.7 | 2.1 |
| Mavazi na Viatu | 6.3 | 0.1 | 0.0 | 0.3 | 0.0 | 5.6 | 5.8 |
| Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyingine | 25.8 | 3.6 | -0.6 | -1.0 | 7.3 | 1.1 | -3.3 |
| Samani, Vifaa vya Nyumbani na Matengenezo ya Kawaida ya Nyumba | 4.8 | 0.2 | 0.0 | -0.2 | 1.3 | 3.7 | 3.2 |
| Afya | 1.3 | 0.0 | 0.0 | -0.1 | -2.1 | 1.6 | 1.5 |
| Uchukuzi | 9.1 | -0.5 | 0.4 | -0.3 | 1.2 | 2.2 | 2.4 |
| Taarifa na mawasiliano | 4.2 | 0.0 | 0.0 | -0.4 | 1.7 | 2.7 | 2.3 |
| Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.1 | 0.0 | 1.9 | -0.5 | 3.8 | 6.2 | 5.7 |
| Elimu | 1.6 | 0.0 | 0.0 | -0.6 | 0.6 | 3.8 | 3.1 |
| Huduma za Migahawa na Malazi | 1.4 | 0.0 | 0.0 | 0.3 | 15.7 | 1.6 | 1.9 |
| Bima na Huduma za Fedha | 0.5 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Huduma binafsi, Ulinzi wa Kijamii na Bidhaa na Huduma Mbalimbali | 1.7 | 0.0 | 0.4 | -0.4 | 0.3 | 5.8 | 5.4 |
| Mfumuko wa bei wa jumla | 100.0 | 0.1 | 0.2 | 0.1 | 5.8 | 3.5 | 3.4 |
| Mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula | 40.5 | -1.6 | 0.7 | 0.6 | 8.2 | 4.1 | 6.4 |
| Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula | 59.5 | 1.5 | -0.2 | -0.4 | 4.1 | 2.9 | 1.0 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo 3.1.1: Mabadiliko ya mfumuko wa bei katika asilimia**

Asilimia




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## 3.2 Bajeti ya Serikali

Mwezi Oktoba 2025, mapato ya Serikali yanayohusisha mapato ya ndani na misaada yalifikia shilingi bilioni 170.8, sawa na asilimia 84.8 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 165, na kiasi kilichobaki kilikua ni misaada. Mapato yanayot okana na kodi yalifikia shilingi bilioni 151.8, sawa na asilimia 88.5 ya lengo, huku mapato yasiyotokana na kodi yakifikia shilingi bilioni 13.2, sawa na asilimia 63.8 (Kielelezo 3.2.1).

**Kielelezo 3.2.1: Mapato ya Serikali**

Shilingi Bilioni




Chanzo: Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar
Tanbihi: Kodi nyingine zinahusisha tozo za hoteli, tozo za wasindikiza wageni, stampu za tozo, tozo za huduma za viwanja vya ndege na bandari, tozo za maendeleo ya barabara na petroli

Kwa mwezi Oktoba 2025, matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 262.1. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 125.1, huku matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 137, ambapo asilimia 83.6 ya kiasi hicho kilitokana na vyanzo vya ndani vya mapato. Mikopo kutoka vyanzo vya ndani vya mapato vilitumika kujaza upungufu wa jumla ya shilingi 91.7 (Kielelezo 3.2.2).

**Kielelezo 3.2.2: Matumizi ya Serikali**

Shilingi Bilioni




Chanzo:Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar
Tanbihi: Matumizi mengine yanahusisha uhamisho wa fedha, malipo ya riba ya deni la ndani, huduma za mfuko mkuu wa serikali na tozo zingine.

## 3.3 Mwenendo wa Sekta ya Nje

### Urari wa Malipo ya Kawaida

Urari wa Malipo ya kawaida uliongezeka kwa asilimia 42.8 hadi kufikia dola za Marekani milioni 649.9 mwaka ulioishia Oktoba 2025. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mapato ya huduma, hususan kutoka kwenye shughuli zinazohusiana na utalii (Jedwali 3.3.1).

**Jedwali 3.3.1: Urari wa malipo**

Dola za Marekani Milioni

| Maelezo | Okt-24 | Sept-25[r] | Okt-25[P] | Mwaka unaoishia Oktoba 2024 | Mwaka unaoishia Oktoba 2025[p] | Ongezeko/ Upungufu (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Urari wa bidhaa (Halisi) | -42.1 | -51.3 | -33.1 | -415.7 | -523.2 | 25.9 |
| Zilizouzwa nje | 10.6 | 6.1 | 7.8 | 59.2 | 32.3 | -45.4 |
| zilizonunuliwa kutoka nje | 52.7 | 57.4 | 40.9 | 474.9 | 555.6 | 17.0 |
| Urari wa huduma (halisi) | 105.7 | 130.1 | 136.6 | 1,047.8 | 1,431.1 | 36.6 |
| Mapato | 116.0 | 139.7 | 144.0 | 1,140.8 | 1,531.9 | 34.3 |
| Malipo | 10.3 | 9.7 | 7.4 | 93.0 | 100.8 | 8.4 |
| Urari wa bidhaa na huduma (halisi) | 63.5 | 78.8 | 103.4 | 632.0 | 907.9 | 43.6 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 126.6 | 145.8 | 151.8 | 1,200.0 | 1,564.3 | 30.4 |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 63.1 | 67.0 | 48.4 | 567.9 | 656.4 | 15.6 |
| Urari wa mapato ya msingi (halisi) | 1.5 | 1.8 | 1.5 | 15.7 | 19.0 | 20.7 |
| Yaliyoingia | 2.2 | 2.3 | 2.2 | 22.9 | 27.3 | 19.0 |
| Yaliyotoka | 0.7 | 0.5 | 0.7 | 7.2 | 8.3 | 15.3 |
| Urari wa uhamishaji Mali (halisi) | 0.1 | 0.2 | 0.2 | 2.1 | 1.8 | -12.8 |
| Iliyoingia | 0.4 | 0.6 | 0.4 | 3.8 | 4.7 | 24.1 |
| Iliyotoka | 0.3 | 0.4 | 0.2 | 1.7 | 2.9 | 69.1 |
| Urari wa Bidhaa,huduma na uhamishaji mali | 65.1 | 80.8 | 105.2 | 649.9 | 928.2 | 42.8 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, benki na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.
Tanbihi: p inaashiria Takwimu za awali; fob, ‘freight on board’.

### Uuzaji wa Bidhaa Nje

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 30.4 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,564.3, ikilinganishwa na kiasi kilichorekodiwa katika mwaka ulioishia Oktoba 2024. Mapato yanayotokana na huduma yameendelea kuimarika yakichangia takribani asilimia 98 ya jumla ya mauzo ya nje ya bidhaa na huduma (Jedwali 3.3.1). Mapato ya huduma yalichangiwa na ongezeko la asilimia 27.9 la idadi ya watalii waliowasili hadi kufikia wageni 902,265 mwaka ulioishia Oktoba 2025. Kwa upande mwingine, thamani ya mauzo ya karafuu nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 50.7 hadi dola za Marekani milioni 10.9,

ikilinganishwa na kiasi kilichorekodiwa mwaka 2024. Kushuka kwa kiwango hiki kulitokana na uzalishaji mdogo unaosababishwa na tabia ya mzunguko wa mavuno wa zao hilo (Jedwali 3.3.2). Kwa ulinganifu wa kila mwezi, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 151.8 kutoka dola za Marekani milioni 126.6 zilizorekodiwa Oktoba 2024.

**Jedwali 3.3.2: Uuzaji wa Bidhaa**

Dola za Marekani Milioni

| Maelezo | Okt-24 | Sep-25 | Okt-25$^P$ | Mwaka unaoishia Oktoba 2024 | Mwaka unaoishia Oktoba 2025$^p$ | Ongezeko/ Upungufu (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa za Mtaji | 14.0 | 13.2 | 9.1 | 51.0 | 76.4 | 49.8 |
| Mitambo na vifaa vya kimitambo | 2.5 | 4.3 | 3.2 | 16.9 | 31.4 | 85.1 |
| Vifaa vya usafirishaji Kiwandani | 9.7 | 2.7 | 1.1 | 17.2 | 16.6 | -3.4 |
| Mashine na Vifaa vya Umeme | 1.3 | 4.3 | 2.7 | 11.1 | 18.1 | 62.4 |
| Bidhaa nyingine za mtaji | 0.5 | 2.0 | 2.1 | 5.8 | 10.4 | 79.9 |
| Bidhaa za uzalishaji wa kati | 32.7 | 33.1 | 23.0 | 361.3 | 400.0 | 10.7 |
| Vifaa vya viwandani | 10.2 | 19.2 | 14.5 | 93.5 | 152.4 | 63.1 |
| Ambazo ni chuma na bidhaa zinazotokana navyo | 0.8 | 6.1 | 3.0 | 22.5 | 30.5 | 35.8 |
| Plastiki na bidhaa zake | 0.7 | 1.7 | 2.0 | 4.6 | 10.5 | --- |
| Mbolea | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | -79.2 |
| Nishati na mafuta | 0.0 | 1.0 | 0.9 | 176.4 | 124.3 | -29.5 |
| ambazo ni bidhaa safi za mafuta | 10.8 | 1.0 | 0.9 | 174.7 | 124.2 | -28.9 |
| Vifaa | 1.8 | 3.8 | 3.4 | 14.2 | 21.4 | 50.1 |
| Chakula na Vinywaji kwa Matumizi ya Viwandani | 9.3 | 7.4 | 3.2 | 62.5 | 80.5 | 28.7 |
| ambazo ni nafaka ya ngano | 5.1 | 3.3 | 0.0 | 22.1 | 22.0 | -0.3 |
| Mafuta ya kula | 3.4 | 3.9 | 0.9 | 25.8 | 38.5 | 49.6 |
| Sukari kwa Matumizi ya Viwandani | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | -13.3 |
| Magari ya matumizi ya nyumbani | 0.6 | 1.5 | 1.1 | 14.7 | 21.4 | 45.6 |
| Bidhaa za Matumizi ya Mwisho | 1.4 | 11.0 | 8.8 | 62.6 | 79.2 | 26.5 |
| Chakula na vinywaji vinavyotumika hasa kwa matumizi ya nyumbani | 0.0 | 1.3 | 1.2 | 15.0 | 16.3 | 9.2 |
| Vifaa vya Usafirishaji Visivyo vya Viwandani | 0.3 | 0.3 | 0.4 | 1.9 | 2.6 | 38.4 |
| ambazo ni pikipiki na baiskeli zilizowekwa na mota ndogo ya ziada | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.8 | 1.0 | 28.6 |
| Bidhaa nyingine za matumizi ya mwisho | 4.4 | 9.4 | 7.1 | 45.7 | 60.2 | 31.8 |
| ambazo ni bidhaa za dawa | 0.7 | 0.0 | 0.1 | 2.3 | 3.8 | 65.6 |
| Dawa za kuua wadudu na bidhaa zinazofanana | 0.0 | 0.1 | 0.1 | 0.5 | 0.4 | -10.5 |
| Sabuni na dawa za kusafisha | 0.4 | 0.7 | 0.2 | 3.6 | 4.9 | 34.1 |
| Vitambaa na Mavazi | 0.4 | 0.8 | 0.8 | 5.6 | 6.1 | 9.1 |
| Viatu na bidhaa nyingine | 0.3 | 0.4 | 0.4 | 2.3 | 3.2 | 43.1 |
| Karatasi na bidhaa zake | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 2.3 | 1.9 | -17.8 |
| Jumla (f.o.b) | 52.7 | 57.4 | 40.9 | 474.9 | 555.6 | 17.0 |

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na uchambuzi wa Benki Kuu ya Tanzania.

## Uagizaji wa Bidhaa kutoka nje

Uagizaji wa bidhaa na huduma uliongezeka kwa asilimia 17.0 hadi kufikia dola za Marekani milioni 555.6 mwezi Oktoba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 474.9 zilizorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (Jedwali 3.3.1). Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kuimarika kwa uagizaji wa bidhaa za mitaji, bidhaa za matumizi ya kawaida, na bidhaa za kati. Uagizaji wa bidhaa za mitaji uliongezeka kwa asilimia 49.8 hadi kufikia dola za Marekani milioni 76.4 kutokana na ongezeko la uagizaji wa mitambo na mashine mbalimbali. Kwa upande wa bidhaa za matumizi ya mwisho, ongezeko lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa vifaa vya usafiri visivyo vya viwandani. Aidha, kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za viwandani ndiko kulikochangia ongezeko la bidhaa za kati (Jedwali 3.3.3). Kwa ulinganifu wa kila mwezi, uagizaji wa bidhaa na huduma ulipungua hadi kufikia dola za Marekani milioni 48.4 kutoka dola za Marekani milioni 63.1 zilizorekodiwa Oktoba 2024.

# VIAMBATISHO

## Jedwali A1: Viashiria vya Kiuchumi

| | | 2020 | 2021 | 2022 | 2023[r] | 2024[p] |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ukuaji wa Pato la Taifa na Mfumuko wa bei | | | | | | |
| 1.1 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika | Asilimia | 8.1 | 7.4 | 9.4 | 10.5 | 9.6 |
| 1.2 Ukuaji halisi wa Pato la Taifa | Asilimia | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1 | 5.5 |
| 1.3 Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika | '000' Sh. | 2,597.7 | 2,705.4 | 2,854.1 | 3,058.8 | na |
| 1.4 Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika | Dola ya Marekani | 1,132.3 | 1,177.4 | 1,239.3 | 1,284.1 | na |
| 1.5 Kasi ya Upandaji Bei | Asilimia | 3.3 | 3.7 | 4.3 | 3.8 | 3.1 |
| 1.6 Uwiano wa Akiba kwa Pato halisi la Taifa (net national disposable income) | Asilimia | 16.5 | 17.3 | 19.7 | 21.9 | na |
| Takwimu za Kifedha na Riba | | | | | | |
| 2.1 Ukuaji wa Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | Asilimia | 5.7 | 15.5 | 11.6 | 14.1 | 11.1 |
| 2.2 Ukuaji wa Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | Asilimia | 8.2 | 17.6 | 12.1 | 11.9 | 9.2 |
| 2.3 Ukuaji wa Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | Asilimia | 7.5 | 23.1 | 7.5 | 8.7 | 11.2 |
| 2.4 Ukuaji Fedha ya msingi (M0) | Asilimia | -4.0 | 17.3 | 15.8 | 3.7 | 19.1 |
| 2.5 Ukuaji wa Mikopo kwa Sekta Binafsi | Asilimia | 3.1 | 10.0 | 22.5 | 17.3 | 12.4 |
| 2.6 Uwiano wa Mikopo kwa Sekta Binafsi kwa pato la taifa[1] | Asilimia | 14.0 | 14.3 | 16.0 | 17.0 | 17.4 |
| 2.7 Uwiano wa Mikopo kwa sekta binafsi kwa mikopo yote | Asilimia | 77.7 | 74.4 | 72.9 | 73.9 | 75.9 |
| 2.8 Riba za Amana za miezi 12 | Asilimia | 8.3 | 8.3 | 8.5 | 8.7 | 9.2 |
| 2.9 Riba za dhamana za serikali kwa ujumla | Asilimia | 4.4 | 4.8 | 4.7 | 7.3 | 10.7 |
| 2.10 Riba ya mikopo ya muda mrefu hadi miaka mitano (3-5 years) | Asilimia | 16.2 | 16.0 | 15.7 | 15.6 | 15.3 |
| Mizania ya Malipo na Nchi za Nje | | | | | | |
| 3.1 Bidhaa Zilizouzwa Nje | Dola Millioni | 6,371.7 | 6,756.2 | 7,223.8 | 7,696.6 | 9,121.6 |
| 3.2 Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje ya Nchi | Dola Millioni | -7,831.7 | -10,003.4 | -14,208.7 | -13,728.9 | -14,278.9 |
| 3.3 Urari wa Biashara | Dola Millioni | -1,460.0 | -3,247.1 | -6,984.9 | -6,032.3 | -5,157.2 |
| 3.4 Urari wa Malipo ya Kawaida | Dola Millioni | -1,458.5 | -2,374.3 | -5,482.2 | -2,960.6 | -2,032.0 |
| 3.5 Urari wa malipo yote | Dola Millioni | -764.9 | 1,852.1 | -988.4 | 52.3 | 80.5 |
| 3.6 Akiba ya Fedha za Kigeni | Dola Millioni | 4,767.7 | 6,386.0 | 5,177.2 | 5,450.1 | 5,546.9 |
| 3.7 Akiba ya fedha za kigeni (miezi) | Miezi | 5.6 | 6.6 | 4.7 | 4.5 | 4.5 |
| 3.8 Kiwango cha kubadili fedha: | | | | | | |
| Wastani wa mwaka | Thamani ya Tshs/Dola | 2,294.1 | 2,297.8 | 2,303.1 | 2,382.1 | 2,597.3 |
| Mwisho wa kipindi | Thamani ya Tshs/Dola | 2,298.5 | 2,297.6 | 2,308.9 | 2,501.4 | 2,374.7 |
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
| Mwenendo wa Mapato na Matumizi | | | | | | |
| 4.1 Uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 15.0 | 13.7 | 14.9 | 15.0 | 15.0 |
| 4.2 Uwiano wa misaada kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 0.7 | 0.5 | 0.4 | 0.3 | 0.3 |
| 4.3 Uwiano wa Matumizi ya kawaida kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 10.1 | 9.9 | 9.8 | 11.0 | 11.0 |
| 4.4 Uwiano wa matumizi ya maendeleo kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | 7.1 | 7.8 | 9.2 | 7.4 | 7.4 |
| 4.5 Uwiano wa nakisi isiyojumuisha misaada kwa Pato la Taifa[1] | Asilimia | -2.2 | -4.0 | -4.1 | -3.4 | -3.4 |
| 4.6 Uwiano wa nakisi ya Jumla kwa Pato la Taifa[1,2] | Asilimia | -1.9 | -4.0 | -3.6 | -3.1 | -3.1 |
| Deni la nje | Dola Millioni | 22,952.7 | 25,519.3 | 27,832.5 | 30,252.7 | 31,950.9 |
| 5.1 Mikopo iliyopokelewa | Dola Millioni | 20,958.4 | 23,250.9 | 25,392.8 | 27,889.3 | 30,416.1 |
| 5.2 Riba ambayo haijalipwa | Dola Millioni | 1,994.3 | 2,268.4 | 2,439.7 | 2,363.4 | 1,534.8 |

Chanzo: Wizara ya Fedha; Benki kuu ya Tanzania; na Mamlaka ya mapato Tanzania

Tanbihi: [1] Imekokotolewa kwa kuzingatia Pato la Taifa kwa bei za miaka husika; [2] inajumuisha misaada, matumizi yaliyochelewa (expenditure float)

n.a - haipatikani, p - ni takwimu za muda

### Jedwali A2: Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Serikali – Tanzania Bara

Shilingi Milioni

| | Bajeti ya 2025/26 | Julai - Septemba 2025 | | Septemba-25 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Makadirio | Halisi | Makadirio | Halisi |
| Mapato ya ndani (yakijumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa) | 40,466,131.4 | 9,198,169.4 | 9,677,845.3 | 3,503,879.5 | 3,718,208.7 |
| Mapato ya Serikali Kuu | 38,785,624.7 | 8,768,964.7 | 9,263,949.6 | 3,352,689.0 | 3,570,397.7 |
| Mapato yatokanayo na kodi | 32,175,999.8 | 7,283,667.5 | 7,962,010.5 | 2,804,596.7 | 3,124,158.0 |
| Ushuru wa forodha | 11,562,965.6 | 2,753,896.1 | 3,014,378.1 | 981,506.5 | 1,051,959.7 |
| Kodi ya bidhaa na huduma | 7,016,470.7 | 1,481,252.5 | 1,561,962.9 | 445,073.0 | 543,935.0 |
| Kodi ya mapato | 11,268,555.1 | 2,502,973.5 | 2,904,532.0 | 1,185,385.1 | 1,354,904.3 |
| Kodi nyingine | 2,328,008.4 | 545,545.4 | 481,137.4 | 192,632.0 | 173,359.0 |
| Mapato yasiyotokana na kodi | 6,609,624.9 | 1,485,297.2 | 1,301,939.2 | 548,092.3 | 446,239.7 |
| Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa | 1,680,506.8 | 429,204.7 | 413,895.6 | 151,190.6 | 147,810.9 |
| Jumla ya matumizi[1] | 48,774,989.1 | 12,743,671.1 | 12,191,059.0 | 4,366,279.6 | 4,284,168.4 |
| Matumizi ya kawaida | 31,281,255.8 | 7,618,379.4 | 7,314,264.8 | 2,563,302.2 | 2,508,580.3 |
| Mishahara | 13,174,240.5 | 3,206,538.2 | 3,223,363.6 | 1,084,708.6 | 1,079,654.8 |
| Malipo ya riba za mikopo | 6,493,715.4 | 1,565,226.4 | 1,242,013.0 | 530,459.8 | 437,308.1 |
| Ya ndani | 3,697,288.1 | 959,508.7 | 800,436.9 | 238,785.4 | 270,703.5 |
| Ya nje | 2,796,427.3 | 605,717.7 | 441,576.0 | 291,674.4 | 166,604.5 |
| Matumizi mengine ya kawaida | 11,613,299.9 | 2,846,614.9 | 2,848,888.2 | 948,133.9 | 991,617.4 |
| Matumizi ya maendeleo | 17,493,733.4 | 5,125,291.7 | 4,876,794.2 | 1,802,977.3 | 1,775,588.1 |
| Fedha za ndani | 12,117,828.4 | 4,254,314.1 | 4,115,312.3 | 1,370,797.0 | 1,461,749.1 |
| Fedha za nje | 5,375,904.9 | 870,977.6 | 761,481.9 | 432,180.3 | 313,839.0 |
| Nakisi ya bajeti bila ya misaada | -8,308,857.7 | -3,545,501.8 | -2,513,213.8 | -862,400.0 | -565,959.7 |
| Misaada | 1,069,884.4 | 199,997.5 | 266,562.2 | 58,854.3 | 43,035.0 |
| Ya bajeti | 113,796.3 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Ya miradi | 846,976.2 | 177,001.7 | 250,378.2 | 51,240.4 | 35,396.0 |
| Ya kisekta | 109,111.9 | 22,995.8 | 16,184.0 | 7,613.9 | 0.0 |
| Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada | -7,238,973.3 | -3,345,504.3 | -2,246,651.5 | -803,545.7 | -522,924.7 |
| Expenditure float | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Marekebisho (Adjustments to cash and other items (net)) | 0.0 | 0.0 | -649,319.5 | 0.0 | 280,068.3 |
| Balansi ya jumla | -7,238,973.3 | -3,345,504.3 | -2,246,651.5 | -803,545.7 | -242,856.5 |
| Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti | 7,238,973.3 | 3,345,504.3 | 2,895,971.0 | 803,545.7 | 242,856.5 |
| Ufadhili kutoka nje halisi | 4,286,343.5 | 679,963.4 | 1,320,618.6 | 238,216.7 | 140,031.1 |
| Mikopo | 8,595,425.8 | 1,215,724.1 | 1,772,575.0 | 373,326.0 | 270,804.0 |
| Mikopo ya bajeti | 1,627,221.4 | 0.0 | 763,792.0 | 0.0 | 0.0 |
| Mikopo ya miradi | 6,968,204.4 | 1,215,724.1 | 1,008,783.0 | 373,326.0 | 270,804.0 |
| ambayo: Mikopo ya masharti ya kibiashara | 2,629,011.8 | 544,744.0 | 513,863.4 | 0.0 | 0.0 |
| Mikopo ya kisekta | 80,624.2 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Marejesho ya mitaji ya mikopo ya nje | -4,389,706.5 | -535,760.8 | -451,956.5 | -135,109.3 | -130,772.9 |
| Ufadhili wa ndani halisi[2] | 2,952,629.8 | 2,665,540.9 | 1,575,352.5 | 565,329.0 | 102,825.4 |
| Mikopo kutoka benki na vyanzo vingine | 2,952,629.8 | 2,665,540.9 | 1,855,691.3 | 565,329.0 | 102,825.4 |
| Mikopo ya benki | 2,466,103.9 | 2,226,320.7 | 392,549.9 | 472,175.7 | -176,003.5 |
| Mikopo toka vyanzo vingine (baada ya marejesho ya mitaji ya mikopo) | 486,526.0 | 439,220.3 | 1,463,141.4 | 93,153.3 | 278,828.9 |
| Mikopo ya ndani (rollover) | 3,325,556.5 | 594,926.3 | 314,587.5 | 133,950.0 | 133,950.0 |
| Kulipa mitaji ya mikopo ya ndani | -3,325,556.5 | -594,926.3 | -594,926.3 | -133,950.0 | -133,950.0 |

Chanzo: Wizara ya Fedha

Note: [1] haijajumuisha marejesho ya mitaji ya mikopo na matumizi yaliyochelewa (expenditure float); [2] thamani chanya ina maana ya ufadhili, na thamani hasi ina maana ya malipo au ongezeko la amana

## Jedwali A3: Tathmini za Amana

Shilingi Bilioni

| Kipengele | Sep-24 | Okt-24 | Nov-24 | Des-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mac-25 | Apr-25 | Mei-25 | Jun-25 | Jul-25 | Ago-25 | Sep-25 | Okt-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Rasilimali halisi za nje | 13,704.3 | 13,773.6 | 13,296.5 | 13,558.2 | 12,688.5 | 14,706.2 | 15,442.1 | 14,658.6 | 14,028.1 | 15,509.5 | 15,726.1 | 15,766.0 | 15,896.7 | 15,715.4 |
| Rasilimali halisi za nje za Benki Kuu | 12,804.0 | 12,668.2 | 11,445.5 | 11,863.4 | 10,927.2 | 13,020.1 | 13,217.7 | 12,273.9 | 11,844.6 | 13,623.0 | 13,884.0 | 13,933.2 | 14,467.3 | 13,334.3 |
| Rasilimali halisi za nje za mabenki | 900.3 | 1,105.4 | 1,851.0 | 1,694.8 | 1,761.4 | 1,686.1 | 2,224.4 | 2,384.7 | 2,183.6 | 1,886.5 | 1,842.1 | 1,832.8 | 1,429.3 | 2,381.1 |
| Rasilimali halisi za ndani | 34,360.2 | 35,469.4 | 36,221.2 | 35,346.8 | 37,146.0 | 35,942.2 | 36,699.8 | 38,679.1 | 39,313.4 | 39,973.8 | 40,565.0 | 41,689.9 | 41,957.4 | 44,091.2 |
| Madai ya ndani | 47,160.9 | 48,136.2 | 48,998.9 | 47,559.0 | 49,255.1 | 48,836.1 | 50,109.3 | 51,989.3 | 52,813.1 | 52,139.4 | 52,548.3 | 54,561.2 | 54,854.2 | 56,509.3 |
| Madai halisi kwa Serikali Kuu | 10,986.7 | 11,618.5 | 12,257.1 | 11,461.6 | 12,679.0 | 11,853.4 | 12,110.0 | 13,233.5 | 13,021.1 | 11,590.4 | 11,576.1 | 13,030.4 | 12,854.4 | 14,122.4 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 36,174.1 | 36,517.8 | 36,741.8 | 36,097.4 | 36,576.1 | 36,982.7 | 37,999.3 | 38,755.8 | 39,792.0 | 40,549.0 | 40,972.2 | 41,530.9 | 41,999.9 | 42,386.9 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 48,064.6 | 49,243.0 | 49,517.7 | 48,905.0 | 49,834.5 | 50,648.4 | 52,141.9 | 53,337.7 | 53,341.5 | 55,483.3 | 56,291.1 | 57,455.9 | 57,854.0 | 59,806.6 |
| Fedha zilizo kwenye mzunguko | 7,353.5 | 7,408.2 | 7,597.1 | 7,351.6 | 6,997.7 | 6,954.5 | 7,190.0 | 7,024.1 | 7,438.9 | 7,874.8 | 8,122.1 | 8,036.4 | 7,730.8 | 8,428.1 |
| Amana za hundi | 22,280.0 | 22,663.5 | 22,617.6 | 22,454.7 | 23,353.0 | 23,777.1 | 24,483.7 | 25,351.5 | 25,031.6 | 25,988.3 | 26,155.4 | 27,442.8 | 28,352.1 | 29,032.2 |
| Amana za akiba na muda maalumu | 18,431.1 | 19,171.3 | 19,303.0 | 19,098.7 | 19,483.8 | 19,916.7 | 20,468.2 | 20,962.1 | 20,871.0 | 21,620.3 | 22,013.5 | 21,976.7 | 21,771.2 | 22,346.4 |
| Fedha taslim (M0) | 11,133.7 | 11,765.8 | 11,859.0 | 12,024.5 | 11,670.3 | 12,078.7 | 11,793.1 | 11,878.9 | 11,800.7 | 12,451.7 | 13,423.8 | 13,537.9 | 13,717.6 | 15,086.7 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 48,064.6 | 49,243.0 | 49,517.7 | 48,905.0 | 49,834.5 | 50,648.4 | 52,141.9 | 53,337.7 | 53,341.5 | 55,483.3 | 56,291.1 | 57,455.9 | 57,854.0 | 59,806.6 |
| Amana za fedha za kigeni (FCD) | 12,427.9 | 12,745.0 | 12,345.2 | 11,765.3 | 12,419.3 | 12,818.2 | 13,605.9 | 13,846.3 | 13,543.4 | 13,769.3 | 13,653.2 | 13,696.3 | 13,337.2 | 13,882.1 |
| *Amana za fedha za kigeni (Dola milioni)* | *4,575.0* | *4,753.2* | *4,708.5* | *4,954.3* | *4,995.3* | *4,951.9* | *5,120.7* | *5,169.1* | *5,045.8* | *5,286.6* | *5,369.8* | *5,560.2* | *5,462.9* | *5,662.4* |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | 35,636.6 | 36,498.0 | 37,172.5 | 37,139.7 | 37,415.2 | 37,830.2 | 38,536.0 | 39,491.4 | 39,798.1 | 41,714.0 | 42,637.9 | 43,759.6 | 44,516.8 | 45,924.5 |
| Amana za akiba na muda maalum zilizo katika shilingi ya Kitanzania | 13,811.2 | 14,224.2 | 14,355.4 | 14,234.2 | 14,342.2 | 14,711.5 | 14,994.3 | 15,478.3 | 15,583.2 | 16,060.1 | 16,406.3 | 16,357.2 | 16,600.4 | 16,848.4 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 21,825.4 | 22,273.8 | 22,817.1 | 22,905.5 | 23,073.0 | 23,118.8 | 23,541.7 | 24,013.1 | 24,214.9 | 25,653.9 | 26,231.6 | 27,402.4 | 27,916.4 | 29,076.1 |
| Fedha zilizo kwenye mzunguko | 7,353.5 | 7,408.2 | 7,597.1 | 7,351.6 | 6,997.7 | 6,954.5 | 7,190.0 | 7,024.1 | 7,438.9 | 7,874.8 | 8,122.1 | 8,036.4 | 7,730.8 | 8,428.1 |
| Amana za hundi | 14,471.9 | 14,865.6 | 15,219.9 | 15,553.9 | 16,075.4 | 16,164.2 | 16,351.7 | 16,989.0 | 16,776.0 | 17,779.1 | 18,109.4 | 19,366.0 | 20,185.6 | 20,648.0 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

# Jedwali A4: Muundo wa Viwango vya Riba

Asilimia

| Kipengele | 2024 Sep | Okt | Nov | Des | 2025 Jan | Feb | Mac | Apr | Mei | Jun | Jul | Ago | Sep | Okt |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A: Riba za mikopo/amana zilizo katika shilingi | | | | | | | | | | | | | | |
| 1. Riba katika soko la fedha baina ya mabenki | | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 1 (*Overnight*) | 7.88 | 7.74 | 7.73 | 7.07 | 7.69 | 7.87 | 7.91 | 7.90 | 7.95 | 7.93 | 6.62 | 6.15 | 6.29 | 6.45 |
| Siku 2-7 | 8.26 | 8.17 | 8.11 | 7.38 | 7.74 | 8.02 | 8.02 | 7.98 | 7.96 | 7.96 | 7.43 | 6.52 | 6.43 | 6.29 |
| Siku 8-14 | 8.51 | 8.81 | 8.23 | 7.68 | 8.51 | 8.62 | 8.21 | 8.08 | 8.28 | 8.12 | 7.57 | 6.71 | 6.93 | 6.92 |
| Siku 15-30 | 9.00 | 9.00 | 9.10 | 9.40 | 8.58 | 8.77 | 8.44 | 8.37 | 8.35 | 6.95 | 7.12 | 6.87 | 7.35 | 7.07 |
| Siku 31-60 | 7.56 | 9.46 | 7.88 | 8.88 | 9.03 | 8.00 | 9.83 | 8.53 | 8.53 | 8.53 | 8.53 | 6.90 | 7.50 | 7.28 |
| Siku 61-90 | 9.50 | 9.50 | 9.00 | 9.00 | 6.75 | 7.00 | 9.83 | 9.11 | 9.14 | 9.14 | 9.14 | 9.14 | 9.14 | 9.14 |
| Siku 91-180 | 9.00 | 10.96 | 7.87 | 7.87 | 7.87 | 10.42 | 10.08 | 12.00 | 12.00 | 12.00 | 11.39 | 7.00 | 7.00 | 9.75 |
| Zaidi ya siku 180 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 | 10.93 |
| Riba ya jumla | 8.16 | 8.04 | 8.06 | 7.41 | 7.80 | 8.06 | 8.12 | 8.00 | 7.98 | 7.94 | 7.35 | 6.48 | 6.45 | 6.38 |
| 2. Riba ya mikopo ya siku 1 kati ya mabenki na | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 7.75 | 7.75 | 7.75 | 7.75 |
| 3. Riba ya mikopo ya muda mfupi toka kwa | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 5.30 | 4.79 | 4.79 |
| 4. Riba ya mikopo ya muda mfupi kwa | 8.00 | 8.00 | 7.72 | 6.26 | 7.21 | 7.21 | 7.21 | 7.21 | 7.21 | 7.21 | 5.77 | 5.78 | 5.76 | 5.76 |
| 5. Riba ya dhamana za serikali | | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 35 | 5.93 | 5.93 | 5.93 | 5.93 | 6.50 | 6.50 | 6.50 | 6.50 | 6.50 | 6.50 | 6.50 | 6.50 | 6.20 | 5.94 |
| Siku 91 | 5.94 | 5.94 | 5.94 | 5.94 | 7.76 | 7.76 | 7.42 | 7.50 | 7.50 | 7.50 | 7.46 | 7.36 | 6.81 | 6.21 |
| Siku 182 | 7.30 | 8.17 | 8.30 | 8.30 | 8.20 | 8.20 | 8.20 | 8.47 | 8.24 | 8.24 | 8.24 | 7.46 | 6.56 | 6.41 |
| Siku 364 | 10.98 | 11.66 | 12.78 | 12.95 | 12.63 | 11.99 | 10.11 | 8.92 | 8.92 | 8.92 | 8.13 | 6.79 | 5.99 | 6.00 |
| Riba ya jumla | 10.85 | 11.55 | 12.68 | 12.95 | 12.51 | 11.93 | 10.10 | 8.86 | 8.89 | 8.89 | 8.13 | 6.83 | 6.03 | 6.27 |
| 6. Riba za hati fungani za serikali | | | | | | | | | | | | | | |
| Miaka miwili | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 12.55 | 12.55 | 12.08 | 12.08 | 12.08 | 12.17 | 12.17 | 12.17 | 10.05 |
| Miaka mitano | 10.09 | 12.41 | 12.41 | 12.41 | 12.41 | 12.41 | 13.14 | 13.14 | 12.94 | 12.94 | 13.18 | 13.18 | 12.48 | 12.48 |
| Miaka saba | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 |
| Miaka kumi | 13.26 | 13.26 | 13.26 | 13.26 | 14.08 | 14.08 | 14.08 | 14.26 | 14.26 | 14.26 | 13.74 | 13.74 | 13.74 | 12.45 |
| Miaka kumi na tano | 15.35 | 15.76 | 15.76 | 15.76 | 15.76 | 15.76 | 14.63 | 14.63 | 14.63 | 14.63 | 14.63 | 13.91 | 13.91 | 13.91 |
| Miaka ishirini | 15.45 | 15.76 | 15.64 | 15.71 | 15.71 | 15.28 | 15.28 | 15.11 | 15.11 | 14.50 | 14.50 | 14.50 | 13.55 | 13.55 |
| Miaka ishirini na tano | 15.42 | 15.42 | 15.93 | 15.93 | 15.84 | 15.84 | 15.84 | 15.84 | 15.29 | 14.80 | 14.80 | 14.42 | 13.19 | 13.19 |
| 7. Riba inayotumika kutathmini dhamana | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.50 | 8.25 | 8.25 | 8.25 | 8.25 |
| 8. Riba za amana za akiba | 2.84 | 2.85 | 2.69 | 2.84 | 2.97 | 2.98 | 2.86 | 2.89 | 2.52 | 2.90 | 2.90 | 2.90 | 2.92 | 2.93 |
| 9. Riba za jumla za amana za muda maalum | 8.20 | 8.25 | 8.18 | 8.33 | 8.31 | 8.13 | 8.00 | 7.82 | 8.58 | 8.74 | 8.83 | 8.61 | 8.50 | 8.36 |
| Mwezi 1 | 9.05 | 9.49 | 10.62 | 10.68 | 9.60 | 9.90 | 9.88 | 7.94 | 10.47 | 9.90 | 11.50 | 10.70 | 9.65 | 9.10 |
| Miezi 2 | 8.35 | 8.55 | 8.14 | 8.90 | 9.61 | 9.02 | 8.81 | 8.78 | 9.25 | 9.85 | 10.75 | 10.07 | 9.28 | 10.09 |
| Miezi 3 | 8.87 | 8.68 | 8.91 | 9.26 | 8.84 | 9.24 | 9.42 | 9.43 | 9.85 | 11.12 | 10.19 | 8.59 | 9.61 | 9.38 |
| Miezi 6 | 9.15 | 9.30 | 9.19 | 9.30 | 9.86 | 9.40 | 9.68 | 9.36 | 9.82 | 10.28 | 10.28 | 10.44 | 10.12 | 10.06 |
| Miezi 12 | 9.12 | 10.41 | 9.63 | 9.62 | 10.08 | 9.48 | 8.14 | 9.27 | 9.72 | 9.79 | 9.88 | 9.99 | 9.84 | 9.21 |
| Miezi 24 | 10.02 | 8.44 | 8.29 | 7.71 | 7.23 | 6.94 | 6.90 | 6.66 | 7.49 | 6.95 | 5.99 | 7.16 | 7.63 | 7.05 |
| 10. Riba za amana kwa wateja wakubwa | 9.88 | 10.27 | 10.14 | 10.39 | 11.80 | 11.40 | 10.35 | 10.52 | 10.64 | 11.21 | 10.72 | 10.99 | 11.05 | 11.22 |
| 11. Wastani wa riba za mikopo | 15.54 | 15.67 | 15.67 | 15.71 | 15.73 | 15.14 | 15.50 | 15.16 | 15.18 | 15.23 | 15.16 | 15.07 | 15.18 | 15.19 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 15.67 | 16.06 | 15.56 | 15.74 | 15.70 | 15.77 | 15.83 | 16.15 | 15.96 | 15.69 | 15.51 | 15.64 | 15.52 | 15.50 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 15.97 | 16.25 | 16.93 | 16.79 | 16.89 | 16.06 | 16.56 | 16.33 | 16.35 | 16.49 | 16.41 | 16.45 | 16.26 | 16.42 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 16.26 | 16.48 | 16.36 | 16.21 | 16.35 | 15.53 | 16.44 | 15.25 | 15.24 | 15.38 | 15.22 | 15.01 | 15.19 | 15.13 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 15.20 | 15.06 | 15.17 | 15.24 | 15.25 | 14.09 | 14.32 | 13.88 | 14.19 | 14.35 | 14.39 | 14.02 | 14.26 | 14.24 |
| Muda mrefu (Zaidi ya Miaka 5) | 14.59 | 14.50 | 14.35 | 14.58 | 14.45 | 14.25 | 14.36 | 14.19 | 14.17 | 14.25 | 14.28 | 14.22 | 14.66 | 14.68 |
| 12. Riba za mikopo kwa wateja wakubwa | 12.92 | 12.93 | 12.77 | 12.83 | 12.80 | 13.42 | 12.94 | 12.88 | 12.99 | 12.68 | 12.56 | 12.72 | 12.84 | 12.40 |
| B: Fedha za kigeni | | | | | | | | | | | | | | |
| 1. Riba za amana | | | | | | | | | | | | | | |
| Amana za akiba | 0.91 | 0.73 | 0.71 | 0.81 | 0.90 | 0.76 | 0.77 | 0.53 | 1.33 | 0.89 | 0.83 | 0.93 | 0.98 | 1.75 |
| Riba za jumla za amana za muda maalum | 3.68 | 3.85 | 3.99 | 4.20 | 4.22 | 3.66 | 2.98 | 2.94 | 3.65 | 3.60 | 3.75 | 4.11 | 3.94 | 4.17 |
| Mwezi 1 | 4.37 | 3.31 | 3.13 | 3.58 | 4.36 | 3.52 | 3.01 | 2.43 | 2.46 | 2.47 | 2.50 | 2.46 | 2.46 | 2.44 |
| Miezi 2 | 2.39 | 3.56 | 3.84 | 4.72 | 4.77 | 3.50 | 2.34 | 2.08 | 3.54 | 3.52 | 3.02 | 4.02 | 4.98 | 4.93 |
| Miezi 3 | 3.88 | 3.93 | 4.97 | 4.79 | 4.47 | 3.31 | 2.23 | 3.62 | 3.53 | 3.03 | 4.31 | 4.98 | 2.56 | 4.55 |
| Miezi 6 | 4.54 | 4.59 | 4.44 | 4.36 | 3.89 | 4.11 | 3.81 | 3.55 | 4.61 | 4.92 | 4.94 | 4.60 | 5.10 | 5.05 |
| 9 months | 3.21 | 3.83 | 3.57 | 3.54 | 3.62 | 3.88 | 3.50 | 3.01 | 4.10 | 4.06 | 4.00 | 4.47 | 4.61 | 3.86 |
| Miezi 12 | 8.44 | 8.77 | 8.53 | 8.80 | 8.83 | 8.97 | 8.93 | 8.89 | 8.81 | 8.70 | 8.82 | 8.59 | 8.43 | 8.71 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 9.41 | 9.50 | 9.50 | 9.44 | 9.89 | 9.93 | 9.99 | 9.97 | 9.99 | 9.93 | 9.91 | 9.89 | 9.89 | 9.88 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 6.75 | 7.60 | 7.74 | 7.78 | 7.58 | 7.64 | 7.94 | 8.16 | 8.39 | 8.22 | 8.23 | 8.11 | 7.49 | 7.73 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 8.70 | 8.76 | 8.02 | 9.19 | 8.81 | 8.57 | 8.28 | 8.23 | 8.49 | 6.88 | 7.03 | 7.16 | 7.25 | 7.43 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 7.52 | 8.23 | 8.01 | 8.23 | 8.18 | 9.11 | 8.61 | 8.36 | 8.17 | 9.43 | 9.42 | 9.30 | 9.16 | 9.23 |
| Muda mrefu (zaidi ya miaka 5) | 9.82 | 9.76 | 9.36 | 9.34 | 9.70 | 9.62 | 9.83 | 9.70 | 9.01 | 9.06 | 9.52 | 8.49 | 8.35 | 9.28 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali A5: Mizania ya Malipo ya Nje

Dola za Marekani (milioni)

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024p |
|---|---|---|---|---|---|
| **A. Urari wa Malipo ya Kawaida** | **-1,458.5** | **-2,374.3** | **-5,482.2** | **-2,960.6** | **-2,032.0** |
| Bidhaa: Zilizouzwa nje ya nchi (f.o.b) | 6,371.7 | 6,756.2 | 7,223.8 | 7,696.6 | 9,121.6 |
| Bidhaa asilia | 808.1 | 627.9 | 766.5 | 953.3 | 1,473.3 |
| Bidhaa zisizo asilia | 5,253.3 | 5,763.0 | 6,058.4 | 6,321.6 | 7,228.8 |
| kati ya hizo: Dhahabu | 2,957.5 | 2,737.1 | 2,835.1 | 3,058.9 | 3,419.6 |
| Bidhaa zisizo rekodiwa | 310.4 | 365.4 | 399.0 | 421.6 | 419.6 |
| Bidhaa: Zilizoagizwa kutoka nje ya nchi (f.o.b) | -7,831.7 | -10,003.4 | -14,208.7 | -13,728.9 | -14,278.9 |
| *Urari wa Biashara ya Bidhaa* | -1,460.0 | -3,247.1 | -6,984.9 | -6,032.3 | -5,157.2 |
| Huduma: Mapato | 2,183.8 | 3,117.7 | 4,762.0 | 6,231.7 | 6,899.4 |
| Usafirishaji | 1,281.7 | 1,558.1 | 1,872.0 | 2,333.4 | 2,356.6 |
| Utalii | 714.5 | 1,310.3 | 2,527.8 | 3,373.8 | 3,903.1 |
| Nyingine | 187.5 | 249.3 | 362.2 | 524.4 | 639.7 |
| Huduma: Malipo | -1,319.0 | -1,607.0 | -2,465.4 | -2,395.9 | -2,608.9 |
| Usafirishaji | -607.0 | -806.4 | -1,378.4 | -1,326.4 | -1,374.5 |
| Utalii | -203.8 | -196.2 | -357.5 | -477.2 | -446.1 |
| Nyingine | -508.2 | -604.4 | -729.5 | -592.3 | -788.4 |
| *Urari wa Biashara ya Huduma* | 864.7 | 1,510.7 | 2,296.6 | 3,835.9 | 4,290.5 |
| *Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma* | -595.2 | -1,736.4 | -4,688.3 | -2,196.5 | -866.7 |
| Mapato ya vitega uchumi: Yaliyoingia | 111.2 | 102.5 | 183.9 | 301.2 | 356.4 |
| Malipo ya Vitega Uchumi: Yaliyotoka | -1,375.7 | -1,294.2 | -1,577.1 | -1,797.7 | -2,098.4 |
| *Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi* | -1,264.5 | -1,191.6 | -1,393.2 | -1,496.6 | -1,742.0 |
| *Urari wa Bidhaa, Huduma na Mapato ya Vitega Uchumi* | -1,859.8 | -2,928.0 | -6,081.5 | -3,693.1 | -2,608.7 |
| Mapato ya Uhamisho Mali wa kawaida: Yaliyoingia | 453.9 | 640.1 | 716.5 | 1,280.9 | 1,177.4 |
| Serikali | 141.2 | 104.7 | 76.4 | 131.0 | 139.2 |
| Taasisi za zisizo za serikali | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Malipo ya Uhamisho Mali wa kawaida: Yaliyotoka | -52.7 | -86.4 | -117.2 | -548.4 | -600.7 |
| *Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida* | 401.2 | 553.7 | 599.3 | 732.5 | 576.7 |
| **B. Urari wa Uhamisho Mitaji** | **344.3** | **412.1** | **274.0** | **223.4** | **318.7** |
| Uhamisho wa Mitaji: Ulioingia | 344.3 | 412.1 | 274.0 | 223.4 | 318.7 |
| Serikali | 270.4 | 346.8 | 208.7 | 158.0 | 253.4 |
| Taasisi za zisizo za serikali | 73.9 | 65.3 | 65.3 | 65.3 | 65.3 |
| Uhamisho wa Mitaji: Uliotoka | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Jumla, A na B | -1,114.2 | -1,962.1 | -5,208.2 | -2,737.2 | -1,713.3 |
| **C. Urari katika Uwekezaji** | **910.0** | **4,037.1** | **3,634.7** | **3,629.9** | **1,383.0** |
| *Uwekezaji wa Moja kwa Moja* | -943.8 | -1,190.5 | -1,437.6 | -1,648.9 | -1,717.6 |
| *Uwekezaji wa Hisa* | -3.6 | -7.9 | 24.6 | 13.9 | -26.1 |
| *Uwekezaji Mwingine* | -30.1 | 2,854.5 | 2,172.5 | 1,967.1 | -308.4 |
| Mali (assets) | -19.8 | -89.8 | 193.0 | -749.6 | -1,255.6 |
| Madeni (liabilities) | -10.3 | 2,944.3 | 1,979.6 | 2,716.6 | 947.1 |
| *Jumla, Makundi A hadi C* | -204.2 | 2,074.9 | -1,573.4 | 892.7 | -330.3 |
| **D. Makosa na Masahihisho** | **-560.7** | **-222.8** | **585.0** | **-850.8** | **410.8** |
| *Urari wa Malipo Yote* | -764.9 | 1,852.1 | -988.4 | 41.9 | 80.5 |
| **E. Akiba ya fedha za kigeni** | **764.9** | **-1,852.1** | **988.4** | **-41.9** | **-80.5** |
| **Vipengele vya Kumbukumbu** | | | | | |
| Uwiano wa Urari wa Malipo ya Kawaida kwa Pato la Taifa | -2.3 | -3.5 | -7.4 | -3.8 | -2.6 |
| Akiba ya Fedha za Kigeni | 4,767.7 | 6,386.0 | 5,177.2 | 5,440.1 | 5,546.9 |
| Akiba ya Fedha za Kigeni (Miezi ya Uagizaji wa Bidhaa Nje) | 5.4 | 4.9 | 4.2 | 4.2 | 4.4 |
| Kiwango cha Kubadilisha Fedha (mwisho wa kipindi) | 2,298.5 | 2,297.6 | 2,308.9 | 2,506.0 | 2,374.7 |
| Kiwango cha Kubadilisha Fedha (Kwa wastani kwa mwaka) | 2,294.1 | 2,297.8 | 2,303.0 | 2,382.1 | 2,597.3 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Ukokotoaji wa Benki Kuu ya Tanzania.
Tanbihi: p inaashiria takwimu za awali; “---“, badiliko linalozidi asilimia 100; f.o.b Mzigo ndani ya chombo

## Jedwali A6: Mauzo ya Bidhaa Nje ya Nchi

**Dola za Marekani(Milioni)**

| | Mwaka unaoishia Oktoba | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025p |
| Bidhaa asilia | 672.7 | 742.7 | 910.2 | 1,148.3 | 1,438.2 |
| Korosho | 198.0 | 230.1 | 170.2 | 297.2 | 450.0 |
| Karafuu | 47.3 | 41.1 | 22.7 | 25.2 | 10.7 |
| Kahawa | 152.5 | 151.7 | 228.6 | 257.2 | 333.4 |
| Pamba | 89.4 | 106.3 | 96.7 | 75.2 | 95.8 |
| Katani | 19.1 | 23.4 | 22.5 | 21.7 | 34.4 |
| Chai | 32.0 | 30.7 | 32.1 | 20.3 | 16.4 |
| Tumbaku | 134.4 | 159.3 | 337.4 | 451.6 | 497.6 |
| Bidhaa zisizo asilia | 5,708.8 | 6,035.4 | 6,352.9 | 6,922.7 | 8,337.5 |
| Madini | 3,115.5 | 3,373.7 | 3,543.3 | 3,972.7 | 5,222.5 |
| Dhahabu | 2,838.5 | 2,813.9 | 2,998.9 | 3,308.9 | 4,596.5 |
| Almasi | 3.8 | 58.6 | 28.8 | 51.3 | 44.1 |
| Tanzanite | 26.9 | 27.7 | 21.3 | 21.1 | 16.9 |
